


**NYONGEZA** ya likizo wazazi watoto njiti yapendekezwa

UKURASA 2

**MAAGIZO** matano muhimu serikali matumizi nishati safi ya kupikia

UKURASA 4

**WATAJA** sababu sita mdororo wa uchumi kwa vyombo vya habari

UKURASA 4

epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe

Jumamosi Novemba 9, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • Na. 0581855

epaper.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US 0745 700 710 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital

## UCHAGUZI MITAA

# VILIO KWA WAPINZANI

**WADAI** wagombea wao kukatwa, Mchengerwa atoa neno, CCM yasisitiza haki... *Endelea ukurasa wa 3*



Katibu wa NEC ya CCM, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla



Kiongozi wa ACT- Wazalendo, Dorothy Semu



Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe



Waziri wa TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa

## Wastaafu sasa kujihakiki kwa simu za mkononi

UKURASA 2




Skani hapa kutembelea chaneli yetu

## Wataalamu waonya matumizi holela dawa

UKURASA 2

MICHEZO GAMONDI ABEBA LAWAMA YANGA UK. 24 KATUNI UK. 6

# Yapendekezwa nyongeza likizo wazazi watoto njiti

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MUSWADA wa Sheria ya marekebisho ya Sheria za Kazi wa Mwaka 2024 umesomwa bungeni na miongoni mwa mapendekezo ni kuongeza muda wa likizo ya uzazi kwa mwajiriwa aliyejifungua mtoto njiti.

Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini, Sura ya 366, Sheria ya Taasisi za Kazi, Sura ya 300 na Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni, Sura ya 436.

Muswada huo ambao umesomwa kwa mara ya kwanza bungeni kwa ajili ya hatua za utungaji wa sheria, kifungu cha 33 kinapendekeza kurekebishwa ili kuongeza muda wa likizo hiyo kwa kujumuisha katika likizo yake ya uzazi muda uliobaki kufikia 36 za ujauzito.

Lengo la marekebisho hayo ni kulinda ustawi na afya za watoto wanaozaliwa kabla ya wakati na kuhitaji muda wa kutosha wa uangalizi wa mama.

Aidha, kifungu cha 34A kinapendekezwa kuongezwa ili kumwezesha mwajiri kumpatia mwajiriwa likizo bila malipo isiyozidi siku 30, lengo ni kuweka mazingira mazuri yatakayomwezesha mwajiriwa kupata likizo bila malipo kutokana na majanga au dharura zinazoweza kujitokeza.

**AJIRA ZA MKATABA**

Pamoja na hayo, kifungu cha 14 kinapendekezwa kurekebishwa ili kubainisha aina ya mikataba ya muda maalum ili kuongeza wigo wa mazingira ambayo mtu anaweza kuajiriwa kwa mkataba wa kipindi maalum, ikiwamo mikataba ambayo mwajiriwa anaajiriwa kwa muda ili kuendana na ongezeko la wingi wa kazi, kutoa fursa kwa wahitimu wa vyuo ili kuwajengea uwezo na kufanya kazi nyingine za misimu.

Kifungu cha 16A kinapendekezwa kuongezwa ili kubainisha mazingira ambayo mwajiri na mwajiriwa wanaweza kuingia katika makubaliano ya namna watakavyofanya kazi katika hali ya dharura inayoweza kuathiri uzalishaji mahali pa kazi.

Lengo ni kuhakikisha ulinzi wa ajira na usalama wa mfanyakazi mahali pa kazi, kuwezesha uzalishaji na kupunguza athari kwa waajiri wakati wa magonjwa ya milipuko na matukio ya dharura.

**MIGOGORO YA KAZI**

Pia kifungu cha 37 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka masharti yanayozuia mwajiri kutoanzisha au kuendelea na shauri la nidhamu dhidi ya mwajiriwa pale ambapo mgogoro huo upo mbele ya Tume au Mahakama ya Kazi.

Lengo ni kuzuia uingiliaji wa mchakato wa ushughulikiaji wa migogoro iliyowasilishwa kwenye Tume au Mahakama ya Kazi.

Aidha, kifungu cha 40 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha fidia kulingana na aina ya mgogoro na kuweka ukomo wa juu wa fidia inayotolewa kwa mwajiriwa aliyeachishwa kazi isivyo halali.

Lengo ni kuweka mwongozo wa utoaji fidia na kudhibiti utoaji wa fidia kwa kiwango kisicho na uhalisia pale inapothibitika kuwa mwajiriwa aliachishwa kazi isivyo halali.

Kifungu cha 41A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti kuhusu afua kwa uvunjaji wa mkataba wa ajira ya muda maalumu na lengo ni kutoa mwongozo wa utoaji wa fidia kwa mwajiriwa pale ambapo mwajiri atakiuka vipengele muhimu vya mkataba vinavyoweza kupelekea mwajiriwa kuacha kazi.

Katika kifungu cha 71 inapendekezwa kuweka masharti ya utaratibu wa kuanza kutumika kwa mikataba ya hali bora inayoingiwa na wakuu wa taasisi za umma na lengo ni kuwianisha masharti ya sheria zinazosimamia utumishi wa umma.

**AJIRA KWA WAGENI**

Katika Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni, Sura ya 436, kifungu cha tisa kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti ya kumtaka raia wa kigeni mwenye kibali cha kazi daraja A anayekusudia kujihusisha na kampuni nyingine anayomiliki hisa kupata idhini ya Kamishna wa Kazi.

Lengo ni kuondoa usumbufu na kuweka mazingira bora ya uwekezaji kwa mwekezaji ambaye ni raia wa kigeni ambapo mara baada ya kupata kibali cha kazi kwa kampuni moja hatahitajika kupata kibali kingine kwa kampuni nyingine atakayomiliki hisa.

Kifungu cha 12 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwawezesha wakimbizi wenye hadhi stahiki kuendelea kufanya kazi bila kubanwa na sharti la ukomo wa muda wa kibali cha kazi.

Vilevile, kifungu hicho kinarekebishwa ili maombi ya kuhuisha kibali cha kazi kuwasilishwa kwa Kamishna wa Kazi angalau miezi miwili kabla ya kuisha kwa muda wa kibali.

# Wataalam waonya matumizi holela ya dawa

**Na Christina Mwakangale**

WATAALAMU wa maabara, wauguzi, wafamasia na madaktari, wametakiwa kuzingatia utaratibu wa utoaji wa dawa kwa wagonjwa, ili kuondoa athari za matumizi holela ya dawa, hasa aina ya antibiotiki.

Mkurugenzi wa Huduma Shirikishi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Mbonea Yonazi, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akifunga mafunzo ya siku mbili ya wataalamu hao kutoka hospitali tisa nchini, baada ya mafunzo ya kusimamia matumizi sahihi ya dawa.

Alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa wataalamu hao ambao moja kwa moja hutoa huduma kwa wagonjwa hususani dawa aina ya antibiotiki, akisema yasipokuwa na matumizi sahihi hugeuka kuwa sugu katika ugonjwa na kusambaza na bakteria. "Mfano unakuta mtu akiumwa kikohozi akapewa dawa za siku saba au nane, zisipofanya kazi tunarudi katika uchunguzi. Baadaye unakuja kubaini sababu ni dawa zimeshajenga usugu. Vimelea vya ugonjwa vikiwa sugu, tiba yake ni changamoto," alisema Dk. Yonazi.

Pia alisema mafunzo hayo yalilenga kutoa mbinu za kudhibiti maambukizi katika hospitali, akisema mgonjwa anapofika na ugonjwa aina moja na kulazwa hospitalini, atibiwe na kupona badala ya kuondoka na magonjwa mengine.

Bingwa wa Maradhi ya Ndani kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja, Zanzibar, Dk. Salma Hashoul Nassor, alisema mbinu zilizotolewa katika mafunzo hayo, zitaboresha majukumu yao katika vituo na hospitali.

Washiriki wa mafunzo hayo, akiwamo Dk. Salma ambaye pia ni Mwenyekiti Kamati inayosimamia, Kudhibiti na Utumiaji Sahihi wa Dawa za Antibiotiki, alisema kutokana na ongezeko la upingamizi wa dawa utokanao na usugu wa dawa, elimu hiyo ni sahihi kwa sasa.

Mfamasia kutoka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kagera ya Bukoba, Tatu Ibrahimu, alisema kutokana na baadhi ya watu kuchukua uamuzi wa kununua dawa kiholela bila kufuata utaratibu, inasababisha vimelea vya magonjwa kuwa sugu.

Dk. Rukia Ibrahim kutoka Hospitali ya Rufani Mkoa wa Singida, Idara ya Watoto, alisema kwa mujibu wa takwimu za dunia, zinakadiria ifikapo mwaka 2050, usugu wa vimelea dhidi ya dawa itakuwa janga la dunia.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akisoma hotuba ya kuahirisha Mkutano wa 17 wa Bunge la 12, jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM**

# Wastaafu kujihakiki sasa kidijitali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa serikali inatengeneza mfumo wa kidijitali utakaowawezesha wastaafu wanaolipwa na Hazina kujihakiki wenyewe kupitia simu zao za mkononi au kwa kutumia huduma za kibenki.

Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Nachingwea (CCM), Amandus Chinguile, aliyetaka kujua kwanini serikali isiweke utaratibu wa wastaafu kuhakikiwa katika halmashauri au kata badala ya utaratibu wa sasa wa kuhakikiwa mkoani.

Alisema uhakiki wa wastaafu wanaolipwa na Hazina umekuwa ukifanyika katika ngazi ya halmashauri na hata hivyo, ili kupunguzia gharama za wastaafu kwenda kujihakiki na kuwaondolea usumbufu wa kusafiri umbali mrefu ili kupata huduma hiyo, serikali inatengeneza mfumo huo.

Chande alisema baada ya kukamilika kwa taratibu zote, wastaafu watapewa elimu ya namna ya kujihakiki wenyewe na watatangaziwa siku ya kuanza kujihakiki. Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alisema kuna wastaafu wanaishi vijijini na ni mbali na makao makuu ya halmashauri na kuhoji, serikali haioni wakati inatengeneza mfumo huo kusogeza huduma kwa wastaafu kwa kutumia watendaji wa kata na vijiji kutokana na hali zao si nzuri.

"Je, ni mshahara gani hutumika kutengeneza pensheni za wastaafu," alihoji.

Naibu Waziri Chande alisema serikali imepokea ushauri wa Mbunge na itakwenda kufanyia kazi na kwamba, mshahara wa mwisho katika utumishi ndio hutumika kutengeneza pensheni kwa mstaafu.



Katibu wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi Taifa (NEC), Itikadi, Uenezi na Mafunzo, CPA Amos Makalla (kulia), akizungumza na Wanachama pamoja na Viongozi wa chama hicho, Wilaya ya Temeke, katika Ukumbi wa PTA Sabasaba, Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Upinzani walia wagombea kuenguliwa

**Na Waandishi Wetu**

VILIO vya wagombea uenyekiti na ujumbe katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kudai kuenguliwa vimetawala katika maeneo mbalimbali nchini.

Pamoja na hali hiyo, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimesisitiza hakitajitoa katika uchaguzi huo, huku ACT-Wazalendo ikisema inaendelea kukusanya taarifa kisha watazitoa.

Chama cha Wananchi (CUF) nacho kimelalamikia wagombea wake kuenguliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) wilaya ya Kinondoni, kimesema hakijapata taarifa za wagombea wake kuenguliwa.

Baadhi ya maeneo mkoani Dar es Salaam ambayo Nipashe imeyatembelea, wagombea wa upinzani wamekutwa wakilia ingawa sababu za kuenguliwa zimeainishwa.

Katika Kata za Makumbusho, Kijitonyama, Hananasifu, Kinondoni, Mwananyamala na Tandale, wagombea pekee waliokuwa wameteuliwa ni wa CCM katika nafasi zote za uenyekiti wa mtaa, ujumbe wa kamati ya mtaa (kundi mchanganyiko) na nafasi ya ujumbe (wanawake).

Miongoni mwa sababu zilizotajwa za baadhi ya wagombea kuenguliwa ni kushindwa kujaza fomu kwa kukosea jina la chama cha mgombea husika, kutojiandikisha kwenye Daftari la Mkazi na kutokujaza anuani ya makazi.

**CHADEMA KUTOJITOA**

Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alisema hadi jana mchana taarifa walizokusanya kutoka mikoa mbalimbali, wagombea wengi wameenguliwa kwa kushindwa kujaza fomu kwa usahihi, kukosa kazi halali za kumwingizia kipato, anuani za makazi, kutumia mhuri ambao haujakamilika.

"Hivi kweli unamwengua mtu eti muhuri haujakamilika au eti ameandika ni mjasiriamali? Hivi walitaka watu waandikaje, wanatafuta visababu ambavyo havina msingi," alisema Mrema.

Alisema pamoja na kuandikwa sababu hizo za kuenguliwa baadhi ya wagombea wake, wasimamizi wa uchaguzi katika mitaa mingi hawakubandika fomu ubaoni zinazoonesha ni namna gani walikosea.

"Kwa hiyo tumewataka wagombea wetu wote ambao majina yao yameenguliwa, kufika katika ofisi za maeneo yao, kushinikiza fomu hizo zibandikwe ili wasome makosa yao na namna ya kujipanga kukata rufani kwa mujibu wa Kanuni ya 23 ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili haki itendeke.

"Kwa sababu wakati wanarejesha fomu za kugombea, nakala moja yenye mhuri walikuwa wanapewa na nyingine inabaki katika ofisi za wasimamizi wa uchaguzi.

"Kwa hiyo fomu zikibandikwa, inakuwa rahisi wao kuona kama hizo ndizo zao au la, kukilinganisha na nakala walizo nazo," alisema Mrema.

Licha ya Mrema kueleza dosari hizo ambazo wanadai kuzibaini, aliapa CHADEMA hakitajitoa katika uchaguzi huo hata kama watabaki na mitaa michache.

"Lakini pamoja na haya yote yanayoendelea, kujitoa katika uchaguzi huu si sehemu ya msamiati wetu. Tutafuata hatua kwa hatua kudai haki itendeke," alisema Mrema.

Aidha, alisema wanaendelea kukusanya taarifa kutoka maeneo mbalimbali na wakikamilisha watatoa taarifa kamili katika vikao vya Kamati Kuu vinavyotarajiwa kukaa hivi karibuni.

Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, kupitia taarifa yake mitandaoni, alisema kinachoendelea katika uteuzi wa wagombea ni ukiukwaji mkubwa wa kanuni, sheria na taratibu na kwamba kinapora demokrasia.

"Madhara ya ubatili huu ni kuendelea kukosekana haki, uhuru na demokrasia ya kweli katika ngazi ya chini zaidi na ya kwanza katika utawala wa nchi. Watanzania wote tunapaswa kutambua wajibu wa kukomesha uporaji wa haki katika uchaguzi huu ambao uko mikononi mwetu," alisema Mbowe.

**ACT KUTOA TAARIFA**

Msemaji wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa ACT Wazalendo, Rahma Mwita, alisema wanalia wagombea wao kuenguliwa kwa sababu ambazo wanazitafsiri kama hujuma.

"Mtu kaandika ni mjasiriamali halafu wao wanasema hiyo sio kazi, hivi kwani hiyo siyo kazi! yaani vitu vidogo vidogo mtu anaondolewa. Huu si uchaguzi ni vurugu kwa sababu walivyojaza wagombea wetu katika hizo fomu ni sawa na walivyojaza wagombea wa CCM ambao wameteuliwa," alidai.

Alitolea mfano wa kata za Makurumla, Kigogo, Ubungo, akisema wagombea wao wote wameenguliwa.

**CUF WAOMBOLEZA**

Hussein Dimoso, ambaye ni mgombea wa CUF katika Mtaa wa Kisiwani kwa nafasi ya uenyekiti, Kata ya Makumbusho, alisema ni mmoja wa ambao hawajateuliwa na sababu iliyotajwa ni kutojaza anuani ya makazi katika fomu yake.

"Ni mara ya tatu kugombea nafasi katika uchaguzi huu na mara zote sikuwahi kujaza anuani ya makazi katika fomu lakini nilikuwa ninateuliwa. Sioni kama hicho ni kigezo kikubwa cha kumwengua mtu.

"Ninafikiri wasimamizi wa uchaguzi, wajitafakari kwa hiki wanachokifanya, kosa la kutokuweka anuani sidhani kama ni kigezo cha kumwengua mtu hasa kama ametimiza sifa za msingi," alisema.

Katibu wa CUF Wilaya ya Kinondoni, Mbaruku Mhina, alisema kitendo cha wagombea wa chama chake kuenguliwa kwa vigezo visivyo na msingi kinasikitisha na kuharibu demokrasia.

**WAPEWA SIKU MBILI**

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uteuzi wa wagombea jijini Dodoma, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mohamed Mchengerwa, alisema wagombea ambao hawajaridhishwa na uteuzi wa nafasi mbalimbali waweke pingamizi ndani ya siku mbili kuanzia jana.

Alisisitiza kwamba uteuzi wa wagombea umefanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 18 ya Tangazo la Serikali namba 571, 573, 574, pamoja na Kanuni ya 17 ya Tangazo la Serikali namba 572 yote ya Julai 12, 2024.

Alisema kwa mujibu wa kanuni hizo,yeyote aliyeomba kuteuliwa kuwa mgombea au mgombea ambaye hakuridhika na uamuzi uliotolewa na msimamizi msaidizi wa uchaguzi, anaweza kuwasilisha pingamizi na kumuomba msimamizi msaidizi wa uchaguzi, kupitia upya uamuzi uliofanyika ili amteue kuwa mgombea au atengue uteuzi anaoupinga.

**IMEANDALIWA na Elizabeth Zaya, Restuta James na Grace Mwakalinga (DAR) na Agusta Njoji (DODOMA)**

## CCM yasisitiza haki kwa vyama vyote

**Na Maulid Mmbaga**

KATIBU wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo, wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Amos Makalla, ametoa msisitizo kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kutenda haki kwa vyama vyote vilivyosimamisha wagombea katika uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji.

Amesema katika uchaguzi huo unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu, wapo wagombea wa CCM ambao wamewekewa pingamizi, hivyo madai ya vyama vya upinzani kwamba wagombea wao pekee ndiyo waliowekewa pingamizi yanalengo la kuwahadaa Watanzania.

Akizungumza na viongozi na wanachama wa CCM wilayani Temeke, mkoani Dar es Salaam jana, Makalla alisisitiza kuwa CCM iko tayari kushiriki uchaguzi huo na kwamba, kitaibuka mshindi kwakuwa kimejiandaa ipasavyo.

"Nitumie nafasi hii kuwaomba TAMISEMI ambao ndiyo wasimamizi wa uchaguzi huu, waitendee haki CCM na vyama vingine vyote vitendewe haki. Tunaamini uchaguzi utakuwa huru na haki na atakayeshinda kwa haki, atangazwe.

"CCM hatuhitaji upendeleo, hatuhitaji kubebwa, tuko tayari tulishajipanga. Hatuhitaji mbeleko na TAMISEMI itende haki kwa vyama vyote vya sisasa vilivyoweka wagombea na sisi tupo tayari kushindana na tutashinda kwa haki," alisema.

Alisema hata wagombea wa CCM wako waliowekewa mapingamizi, lakini vyama vya upinzani vinataka kuwadanganya Watanzania kama vile wagombea wao tu ndiyo waliowekewa mapingamizi.

"Wagombea wa CCM wamewekewa mapingamizi katika baadhi ya maeneo kama vile baadhi ya vyama vingine walivyowekewa mapingamizi. Haiwezekani wakati wagombea wa CCM wamewekewa mapingamizi alafu waoneshe wao tu ndio wamewekewa mapingamizi.

"Juzi nilisema Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, ametamka bayana kwamba CHADEMA hawana uwezo wa kuweka wagombea kila maeneo. Baada ya kusema hivyo sasa wamejipanga kumrushia madongo.

"Mlisikia jana walisema katika Mkoa wa Dar es Salama wameweka wagombea 540 ni waongo, yote ni kumpiga Tundu Lissu na leo ninajua Mnyika ataongea, anataka kutoa takwimu za kusimamisha wagombea za kuwahadaa Watanzania kwamba wamejipanga lakini kumbe ni uongo,"alisema.

Makalla alisema chama hicho kimepoteza muda mwingi katika maandamano, hivyo katika uchaguzi huu hawajajipanga na kina mgogoro mingi ndani.

"Katika chama chao kuna CHADEMA Lissu na CHADEMA Mbowe, wanavutana na ndiyo maana mnawaona hawaongei, hawapo tayari kwenye uchaguzi huu na CCM tutumie nafasi hii kushinda uchaguzi huu.

"Hakuna demokrasia iliyoporwa, Rais Samia Suluhu Hassan kupitia 4R ndiye aliyewaruhusu wafanye mkutano. Ndiye aliyewaruhusu wafanye ziara.

"Hakuna demokrasia iliyoporwa, wanatafuta sababu za kuthibitisha kushindwa kwao mapema. Wanataka kuwahadaa Watanzania kama vile wanaonewa kumbe ni waongo. Chama chao kimepoteza dira na mwelekeo wasitafute kisingizio," alisema Makalla.

# Waonywa ukiukaji matumizi ya fedha

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewataka maofisa masuhuli na watendaji wote serikalini kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za fedha za umma ili kutimiza ndoto na malengo ya kuwaletea Watanzania maendeleo endelevu.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitoa agizo hilo jana wakati akiahirisha Mkutano wa 17 wa Bunge la 12 Bungeni jijini Dodoma.

Alisema lengo la serikali ni kuendelea kutoa huduma bora kwa wananchi kwa kuimarisha utamaduni wa uwajibikaji katika kusimamia na kudhibiti ipasavyo ukusanyaji wa mapato na matumizi.

Majaliwa alisema vikao vya bunge la 12 vilipokea na kujadili kwa kina taarifa za Kamati za Bunge ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 ulioishia Juni 30, 2023.

Waziri Mkuu alisema taarifa hizo za kamati zinazotokana na taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

"Ninalipongeza Bunge lako tukufu kwa kuchambua kwa kina hoja zote za ukaguzi zinazohusu matumizi ya fedha za umma. Pamoja na kutoa maazimio ambayo kimsingi ni maelekezo mahsusi kwa serikali," alisema.

Majaliwa alisema hoja zote zimeainishwa kwa ajili ya utekelezaji, hivyo kuziagiza wizara zote kuandaa kwa wakati taarifa za utekelezaji wa maazimio yote kulingana na mapendekezo yaliyotolewa na kamati za Bunge na kuziwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu ili kuwasilisha taarifa ya serikali kwa Spika.

"Sote ni mashahidi kwamba serikali imeendelea kufanyia kazi mapendekezo yanayotolewa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi chini ya uongozi wa Charles Kichere, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Vilevile, serikali imeendelea kuzingatia maelekezo yote yanayotolewa na Bunge kupitia maazimio na hoja zilizotolewa," alisema.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu aliwapongeza wananchi kwa kujitokeza kwa wingi wakati wa uandikishaji wa wapigakura katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa. "Vilevile, nitoe rai kwa wananchi wote kama walivyojitokeza kwenye kujiandikisha vivyo hivyo wajitokeze siku ya tarehe 27 Novemba, 2024 kupiga kura," alisisitiza.

# Maagizo matano nishati safi ya kupikia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa maelekezo mahsusi matano kwa taasisi, wizara na umma kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia likiwamo ifikapo mwezi ujao.

Katika kutekeleza hilo, ametaka wakuu wa mikoa na wilaya kuonesha ni taasisi ngapi tayari zimetekeleza agizo hilo.

Akiahirisha mkutano wa 17 wa Bunge jana jijini hapa, Majaliwa alisema taasisi zote zenye kuandaa chakula cha watu zaidi ya 100 zinapaswa kutekeleza maagizo ya kuhamia katika matumizi ya nishati safi ya kupikia.

"Wizara ya Nishati iendelee kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia; wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya kote nchini, wafanye ukaguzi katika taasisi zilizomo katika maeneo yao mathalani majeshi na polisi.

"Vyuo vya elimu ya kati na ya juu, vyuo vya wizara mbalimbali kama elimu, afya na kilimo, ambapo yanayopaswa kubadilisha mifumo yao ya nishati ya kupikia kwa vile yana idadi kubwa ya walaji wa vyakula," alisema.

Majaliwa alisema wajasiriamali wanaopika chakula cha watu wengi kama vile katika harusi wahamasishwe ili nao wabadilishe teknolojia zao, ziendane na matumizi ya nishati safi ya kupikia.

"Ninawaelekeza wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya wote ifikapo mwezi Desemba, mwaka huu, watoe taarifa ya utekelezaji kuonesha ni taasisi ngapi tayari zimetekeleza agizo hili.

"Hii ni kwa taasisi zote za umma na binafsi. Lengo ni kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2033 asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia ambayo ni: gesi, umeme, vumbi la makaa ya mawe, Kunipoa zinazotokana na takataka," alisema.

Majaliwa aliwataka wananchi waendelee kubadili mfumo wa maisha hususani taratibu za kupika chakula ili kuachana na nishati chafu ya kupikia inayohusisha kuni na mkaa unaotokana na miti.

Pamoja na hayo, aliagiza wizara zote kuandaa kwa wakati taarifa za utekelezaji wa maazimio yote ya taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kulingana na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati za Bunge, na kuziwasilisha Ofisi ya Waziri Mkuu ili iweze kuwasilisha taarifa ya serikali kwa Spika wa Bunge.

Pia, aliwataka watendaji wote serikalini wahakikishe vipaumbele vilivyoanishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026 vinatafsiriwa vema kwenye mipango ya taasisi zao.

Majaliwa alisema serikali imeendelea kusimamia makusanyo katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2024/25 na Sh. trilioni 11.55 zimekusanywa kutoka vyanzo vya ndani na nje ya nchi.

Alisema mafanikio hayo yanatokana na mikakati mbalimbali iliyowekwa na serikali ikiwamo kuendelea kuimarisha na kuhimiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika ukusanyaji wa mapato na kuhamasisha matumizi ya mashine za kutolea risiti za kielektroniki.



Imamu Mkuu wa Msikiti wa Mnyamani, Buguruni na Mratibu wa Taasisi ya Mashekhe na wanazuoni wa Kiislamu Tanzania, Shekhe Mohamed Idd, akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam juzi, wakati akitoa nasaha kwa baadhi ya viongozi wa dini kutumia maneno ya heshima na hadhi, pale wanapowazungumzia viongozi wa nchi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wataja sababu sita mdororo wa uchumi vyombo vya habari

**Na Jenifer Gilla**

MHADHIRI katika Shule Kuu ya Uandishi wa Habari, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, (SJMC), Abdallah Katunzi, ametaja sababu sita za kuendelea kudorora kwa uchumi wa vyombo vya habari ikiwamo kukua kwa teknolojia.

Zingine amesema ni usimamizi usio mzuri wa biashara, uwekezaji mdogo kwenye sekta, uduni wa maudhui, mfumo wa kodi na madeni.

Akitoa taarifa ya uchumi wa vyombo vya habari Tanzania juzi katika mkutano wa nane wa Jukwaa la Wahariri (TEF) jijini Dar es Salaam, Katunzi alisema, umeshuka kwa asilimia 50.

Katunzi alisema hata uchapishaji wa magazeti umeshuka hali iliyosababisha mapato kupungua na mishahara ya waandishi wa habari kuwa midogo kwa asilimia 29, kulipwa mshahara chini ya Sh. 150,000 na asilimia 31 wakilipwa chini ya Sh. 300,000.

Pia alisema asilimia 17 wanalipwa mshahara usiozidi Sh. 500,000, asilimia 10 wakilipwa usiozidi Sh. milioni mbili, asilimia sita chini ya Sh. 750,000, asilimia tano chini ya Sh. milioni moja na asilimia mbili wakilipwa zaidi ya Sh. milioni mbili.

Alitaja sababu za kushuka kwa uchumi katika sekta hiyo kuwa ni kukua kwa teknolojia kulikosababisha taarifa kusambazwa kwa haraka kupitia mitandao ya kijamii, hivyo njia ya kizamani ya kutoa habari ikiwamo magazeti, redio na televisheni kukosa wateja.

Alitaja sababu nyingine kuwa ni usimamizi duni wa biashara unaotokana na kutokuwapo na wataalam waliobobea wa kuendesha sekta hiyo kisasa ikiwamo uchumi wa kidijitali.

Katunzi alisema pia kwa sasa waandishi wengi wanaandika habari zenye viwango vya chini kutokana na sababu mbalimbali nikiwamo kukosa fedha za utekelezaji na ardhi ya kufanya kazi, hivyo vyombo kukosa habari za uchunguzi wa kina zinazowavutia wasomaji.

Alitaja sababu nyingine kuwa ni vyombo vya habari hasa binafsi kudai fedha nyingi kampuni na taasisi mbalimbali zikiwamo serikali, lakini pia vimeelemewa na madeni kutoka maeneo tofauti kama mifuko ya hifadhi ya kijamii na mifumo ya kodi sі rafiki kwao.

Katika kukabiliana na hali hiyo, Katunzi alishauri vyombo vya habari kutafuta ushauri wa kitaalam wa namna ya kuviendesha vyombo hivyo kisasa, kujikita kwenye uandishi wa miradi ili kupata fedha za kuandika habari za kiuchunguzi.

Alishauri pia kufanya ushirikiano wa kimkakati na taasisi nyingine kama vile wizara na idara mbalimbali na viwekeze katika miradi ya ubunifu kama vile, nishati safi ya kupikia na treni ya kisasa ya mwendokasi (SGR).

# Adaiwa kumbaka kisha kumuua mtoto wa rafiki yake

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MTOTO wa umri wa miaka tisa na mwanafunzi wa darasa la pili shule ya msingi Nabweko, Nansio wilayani Ukerewe mkoani hapa, anadaiwa kukabwa na kubakwa hadi kufa na mtu anayedaiwa kuwa rafiki wa baba yake aliyetambulika kwa jina la Jackson, maarufu kama Mjomba.

Tukio hilo lilitokea Novemba 3, mwaka huu, majira ya saa 2:00 usiku wakati mtoto huyo (jina linahifadhiwa) alipokuwa akicheza na wenzake kisha kuchukuliwa na Jackson kwa ahadi ya kwenda kumnunulia pipi dukani na kutoweka naye kusikojulikana hadi mwili wake ulipopatikana Novemba 4.

Taarifa ya tukio hilo ilitolewa jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Naibu Kamishna (DCP) Wilibroad Mutafungwa, akibainisha kuwa mwili wa mtoto huyo ulipatikana na kutambuliwa na wazazi wake kwenye jengo ambalo halijakamilika kujengwa.

DCP Mutafungwa alisema mwili huo ulikutwa katika jengo hilo ukionekana kubakwa kisha kukabwa katika maeneo ya shingoni hali iliyomsababishia umauti.

"Mtuhumiwa baada ya kutekeleza ukatili huo alitokomea kusikojulikana na tunaendelea kumsaka. Mwili wa marehemu umefanyiwa uchunguzi wa kitaalamu na kukabidhiwa ndugu kwa ajili ya mazishi," alisema DCP Mutafungwa.

Aidha, aliwataka wananchi kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa itakayofanikisha kukamatwa kwa mtuhumiwa huyo popote alipo ili hatua kali za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi yake.

Katika hatua nyingine, DCP Mutafungwa alithibitisha kutokea kwa kifo cha Mariam Marko (27) mkulima na mkazi wa Kongongwe, kata ya Nyanguge, wilaya ya Magu anayedaiwa kunywa sumu Novemba 5, 2024

Alisema Novemba 5, mwaka huu, majira ya saa 9:00 alasiri katika kitongoji cha Kongogwe, katika kituo cha Polisi Nyanguge kuliripotiwa taarifa ya mtu aitwaye Mariam Marko kujaribu kujiua kwa kunywa sumu.

Mariam anadaiwa kufikia hatua hiyo kutokana na msongo wa mawazo baada kutengwa na mume pamoja na ndugu zake kwa madai ya ulevi wa kupindukia.

"Mwili wa Mariam umefanyiwa uchunguzi wa kitaalam na kukabidhiwa ndugu kwa taratibu za mazishi.



Mkurugenzi wa Uchaguzi wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), Kailima Ramadhani (katikati), akizungumza wakati wa mafunzo kuhusu sheria za uchaguzi kwa Wakuu wa Polisi Wilaya, yaliyofanyika katika Shule ya Polisi Moshi, mkoani Kilimanjaro, juzi. Kushoto ni Kamishna wa Polisi Operesheni na Mafunzo, Awadhi Juma Haji na Mkurugenzi wa Huduma za Kisheria wa Tume hiyo, Selemani Mtibora. **PICHA: INEC**

# Masharti mapya kwa utoaji hadhi diaspora

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MUSWADA wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali namba nne wa mwaka 2024, umesomwa kwa mara ya kwanza bungeni ukiwa na mapendekezo mbalimbali yakiwamo masharti kwenye utoaji wa hadhi maalum kwa Diaspora.

Mapendekezo ya muswada yanalenga kufanya marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54 na kifungu cha 28 kwa ajili ya kuongeza masharti mapya ya ruhusa ya kuingia nchini kwa kutumia kadi ya Tanzanite Diaspora na taarifa ya idhini ya kupewa kadi hiyo.

Lengo la marekebisho hayo ni kumwezesha mmiliki wa kadi ya Tanzanite Diaspora na mgeni ambaye ana taarifa ya kuidhinishwa kuingia ndani ya Jamhuri ya Muungano kutumia nyaraka hiyo bila kuathiri takwa la kuwa na pasipoti halali.

Aidha, alisema sheria inapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa kuongeza vifungu vya 36A, 36B, 36C, 36D na 36E kwa ajili ya kuweka masharti yanayohusu hadhi maalum kwa raia wa nchi nyingine ambaye aliwahi kuwa raia wa Tanzania au mwenye asili ya Tanzania.

Masharti hayo pia yanakusudiwa kutumika kwa mtu ambaye alikuwa raia wa Jamhuri ya Muungano, isipokuwa kwa wale waliokuwa na uraia wa kuasili au mtu ambaye mzazi wake mmoja, babu, bibi au mtu yeyote katika kizazi kilichomtangulia ni, au alikuwa raia wa Jamhuri ya Muungano.

Kwa mujibu wa vifungu vipya vinavyopendekezwa, pale ambapo mtu anapewa hadhi maalum, hadhi hiyo itamwezesha kuingia katika Jamhuri ya Muungano na kushiriki katika shughuli za kiuchumi na kijamii.

Aidha, hadhi maalum itaenda sambamba na kupata kadi ya Tanzanite Diaspora ambayo itakuwa ni uthibitisho rasmi kwamba mmiliki wa kadi hiyo ana hadhi maalum.

Vilevile, masharti mapya yanayopendekezwa yanaainisha masuala kuhusiana na muda wa uhalali, wategemezi na masharti na utaratibu wa kufutwa kwa kadi ya Tanzanite Diaspora.

Aidha, Kifungu cha 45 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza neno 'Kadi' ili kuainisha adhabu kwa makosa yatakayotendwa na wamiliki wa kadi ya Tanzanite Diaspora kama ilivyo kwa wamiliki wa visa, vibali, vyeti na hati za kusafiria vinavyotolewa chini ya Sheria.

Kifungu cha 48 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza eneo ambalo Waziri anaweza kulitengenezea kanuni ili kujumuisha utaratibu wa uombaji na utoaji wa hadhi maalumu. Lengo la marekebisho haya ni kuwezesha utekelezaji bora wa masharti ya Sheria.

Kuhusu umiliki wa ardhi, Sehemu ya Saba ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Ardhi, Sura ya 113 ambapo kifungu cha 19 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho kwa lengo la kuweka utaratibu wa matumizi ya ardhi kwa mtu aliyepewa hadhi maalumu chini ya Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54.

Kwa mujibu wa marekebisho yanayopendekezwa, mtu aliyepewa hadhi maalumu atakuwa na haki ya kumiliki ardhi kupitia utaratibu wa hati miliki maalumu itakayotolewa na Kamishna wa Ardhi.

Lengo la marekebisho hayo ni kumwezesha raia wa kigeni mwenye asili ya Tanzania kumiliki au kuondosha miliki ya ardhi aliyoipata kwa njia mbalimbali ikiwemo urithi au kununua.

Hati miliki maalumu itakuwa aina ya hati miliki itakayotolewa kwa vigezo na masharti maalumu.

Aidha, kifungu cha 32 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuainisha muda wa hati miliki maalumu itakayotolewa kwa mtu aliyepewa hadhi maalumu.

Kwa mujibu wa marekebisho haya hati miliki maalumu itakayotolewa na Kamishna wa Ardhi kwa mtu aliyepewa hadhi maalum itakuwa kwa muda usiozidi miaka thelathini na tatu.

Kifungu cha 20A kinapendekezwa kuongezwa na vifungu vya 48 na 49 vinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kuweka utaratibu wa kutoa na kusitisha hati miliki maalumu iliyotolewa kwa mtu aliyepewa hadhi maalumu.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Utulivu, busara zahitajika Ligi Kuu Bara ikishika kasi

**MECHI** za Ligi Kuu Bara zimesimama kwa muda ili kupisha Kalenda ya Kimataifa ambapo kwa Tanzania (Taifa Stars), yenyewe itakuwa na kibarua cha kusaka tiketi ya kufuzu kushiriki fainali ya Kombe la Mataifa Afrika (AFCON 2025) kwa kucheza ugenini dhidi ya Ethiopia hapo Novemba 16, mwaka huu.

Ethiopia wameamua kuipeleka mechi hiyo katika Mji wa Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), kufuatia nyumbani kwao kutokuwa na uwanja wenye ubora unaokubalika na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Baada ya mechi hiyo, Taifa Stars iliyoko Kundi H itarejea nyumbani haraka kuwasubiri Guinea, mchezo utakaofanyika Novemba 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ili kujiweka katika nafasi salama na bila kuangalia matokeo ya mechi nyingine, Taifa Stars iliyoko chini ya Hemed Suleiman 'Morocco' inatakiwa kushinda michezo hiyo miwili wakati tayari DR Congo imeshafuzu kushiriki fainali hizo zitakazofanyika mwakani nchini Morocco.

Kutokana na majukumu hayo ya kimataifa kwa Taifa Stars, Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama na itarejea tena kuanzia Novemba 21, mwaka huu.

Uamuzi wa kusimamisha ligi hiyo ikiwa imeingia katika raundi ya 11, umetokana na Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), kutotaka kuona idadi ya mechi za viporo zinakuwa nyingi kama ilivyowahi kuwa misimu iliyotangulia.

Miaka ya nyuma tulishuhudia timu nyingine ambazo wachezaji wake hawajaitwa katika kikosi cha Stars, wakiendelea na michezo, hali ambayo imekuwa tofauti kwa sasa, timu zimetofautiana mechi moja.

Huku baadhi ya timu zikiwa zimecheza michezo 10 na nyingine chache zimeshuka dimbani mara 11, tayari baadhi ya makocha wameshapoteza ajira zao au wengine wakikalia 'kuti kavu' kutokana na matokeo yasiyoridhisha kwa klabu wanazoziongoza.

Ni kweli makocha wanaajiriwa kwa ajili ya kufukuzwa, na ili wasifukuzwe ni lazima wahakikishe wanazipa matokeo chanya timu wanazoziongoza na kubwa ni kubeba ubingwa.

Na ili timu husika ifikie malengo, ni lazima kila kocha ahakikishe anapata ushindi katika michezo yote bila kujali anakutana na 'mkubwa' mwenzake au timu changa katika mashindano husika.

Tunawakumbusha viongozi, wachezaji, mashabiki na wadau wa mpira wa miguu kufahamu mchezo huo unaopendwa zaidi duniani una matokeo matatu, maana yake kuna kushinda, kupata sare au kupokea kichapo.

Ni kweli makocha na viongozi wa klabu mbalimbali wanakuwa katika hali ya sintofahamu au kikaangoni baada ya timu zao kukosa matokeo mazuri, lakini ili kupata suluhisho la changamoto hiyo, si kuchukua uamuzi wa kufukuza kocha.


Ni vyema kabla ya viongozi wa klabu kuchukua hatua za kufukuza makocha, wakajiuliza zaidi kama matokeo hayo mabaya yamesababishwa na nini, kama walifurahi pamoja walipopata ushindi, basi wakumbuke hata unapotoa sare au kupoteza mchezo, hiyo ni sehemu matokeo katika mpira wa miguu.

Badala ya kukurupuka kuchukua uamuzi wa kumfukuza kocha, tunawashauri viongozi wa timu zote zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kujadiliana ili kufahamu walipoangukia na ligi itakaporejea tena wawe imara.

Tubadilike, hakuna timu inayoshinda mechi zote duniani.

Wakati timu nyingine zitarejea katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara kuanzia Novemba 21, mwaka huu, mabingwa watetezi, Yanga wao watakuwa na kibarua cha kuhakikisha wanaanza vyema mechi za hatua ya makundi kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika huku Simba wakiwakilisha katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

Na Adam Fungamwangwo

# Kichapo mechi mbili isiwe sababu Yanga kuvurugana

**KATIKA** hali isiyo ya kwaida, Yanga imefungwa michezo miwili mfululizo ya Ligi Kuu Tanzania Bara kitu ambacho ni nadra sana kutokea katika mpira wa miguu nchini.

Sikumbuki ni lini si timu kubwa nchini kupoteza michezo ya Ligi Kuu miwili mfululizo. Inawezekana ni zamani sana tangu miaka ya 1980, tena inawezekana ikawa ni Simba ambayo mwaka 1988, na 1989, ilinusurika kushuka daraja, ikipona katika michezo ya mwisho, na hii ilitokana na mgogoro mkubwa wa viongozi.

Kulikuwa na pande mbili zinazovutana, Baraza la Wazee na upande wa aliyekuwa Katibu Mkuu wa klabu hiyo, marehemu, Jimmy Ngonya.

Kwa Yanga bado tunafuatilia rekodi kujua ni mwaka gani ilipoteza michezo miwili mfululizo ya ligi.

Kibaya zaidi imepoteza ikiwa kwenye kilele cha ubora, ikitawala soka ndani na nje ya nchi. Afadhali ingekuwa ina kiwango cha kawaida, lakini kwa misimu miwili imeweza kutawala katika Ligi Kuu Tanzania Bara, pamoja na kulichachafya Afrika kwa kufika fainali ya Kombe la Shirikisho, na msimu uliofuata ikafikia hatua ya robo fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa.

Hii inaonyesha Yanga ni timu iliyo kwenye kiwango cha hali ya juu. Hata hivyo tangu kuanza kwa msimu huu baadhi wachambuzi na watangazaji walianza kutia shaka kiwango cha timu hiyo.

Ilikuwa karibu kupoteza zaidi kuliko kushinda idadi kubwa ya mabao kama ilivyokuwa msimu uliopita.

Wengine wakaenda mbali zaidi ya kusema kama si maamuzi ya kibinadamu ya waamuzi mpaka sasa Yanga ingekuwa imepoteza michezo zaidi ya hiyo miwili.

Jumamosi iliyopita ilichapwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC, kabla ya juzi kuchakazwa mabao 3-1 dhidi ya Tabora United, mechi zote mbili ikiwa mwenyeji.

Baada ya kipigo cha juzi uongozi wa Yanga uliitisha kikao ili kujua nini kimesababisha na hatua za haraka ambazo itachukua ili kuweka mambo sawa kuelekea michezo inayofuata.

Kwanza kabisa niwapongeze viongozi wa klabu hiyo kwa kuitana na kukaa haraka ili kuangalia tatizo linaloikabili, lakini angalizo wasifanye maamuzi kwa mhemko au jazba.

Zipo tetesi ambazo si rasmi kuwa Kocha Mkuu, Miguel Gamondi, amekalia kuti kavu na anaweza 'kunyolewa' wakati wowote.

Binafsi sidhani kama kumwondoa Gamondi kama ambavyo inaelezwa kwenye tetesi kama ni sahihi.

Viongozi wa Yanga inabidi kwanza watafakari ili wajue chanzo cha matatizo yote haya ni nini?

Klabu ya Simba ilichelewa kufanya uamuzi, lakini uchunguzi wao ulikuwa sahihi wachezaji wengi walikuwa wamechoka, umri mkubwa, hawana morali, wameshapata kila kila kitu, mataji pamoja na mishahara mikubwa, hivyo hawana wanachopigania tena.

Kilichofanyika ni kuondoa idadi kubwa ya aina hiyo ya wachezaji wa kusajili nyota wengi vijana ambapo matunda yao yameanza kuonekana kwa sasa ingawa si kwa kiwango kikubwa.

Binafsi nilidhani baada ya kina Stephane Aziz Ki, Pacome Zouzoua, Maxi Nzengeli, Kennedy Musonda na wengine kufanya vyema kwa misimu miwili mfululizo, viongozi wangewatafutia wachezaji vijana ambao wangekuja kuwaongezea nguvu kipindi cha usajili wa dirisha kubwa.

Badala yake wakasajiliwa wachezaji ambao umri ni sawa tu na waliopo Yanga ambao ni Prince Dube, Clatous Chama, Jean Baleke, na si wachezaji wabaya lakini wameingia katika kikosi cha wachezaji ambao tayari wameshapata mafanikio. Kibaya zaidi ni hata wao wenyewe ni wazoefu na wameshapata mafanikio kwenye soka la Bongo wakiwa na timu zingine, hivyo hawajisukumi na kujituma zaidi ili mashabiki wawafahamu kama wale wa Simba.

Kinachotakiwa kwa sasa viongozi wa Yanga, wasitupiane lawama, kufukuza kocha, wala kuvurugana wenyewe kwa wenyewe. Kinachotakiwa ni kipindi cha dirisha dogo kusaka wachezaji wachache wapya kabisa, ambao watakuja kuongeza nguvu, kujituma kusaka ustaa ndani ya kikosi, hivyo kuwasaidia waliopo ambao wameanza kuchoka baada ya kucheza michezo mingi, wakitumia nguvu na akili nyingi na kuipa timu mafanikio makubwa.

# Vijana 5,740 waandikishwa jeshi la JWTZ

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema kuanzia Mwaka 2019 hadi mwaka 2022, vijana 5,744 waliokuwa na sifa waliandikishwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) ikiwa ni pamoja na walioshiriki katika ujenzi wa ukuta wa Mirerani na Ikulu Chamwino.

Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk.Stergomena Tax aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti maalum (CCM), Asia Halamga.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji kuna mpango gani wa kuajiri vijana wa JKT walioshiriki katika ujenzi wa ukuta wa Mererani, Ikulu na maeneo mengine.

Akijibu swali hilo, Tax alisema Jeshi la Kujenga Taifa lilianzishwa mwaka 1963 kwa lengo la kutoa mafunzo ya uzalendo, ulinzi na malezi kwa vijana wa kitanzania.

Alibainisha kuwa mafunzo hayo yanalenga kuwafundisha umoja na mshikamano, ukakamavu na kuwa tayari kulitumikia Taifa lao wakati wote.

"Katika mafunzo hayo, vijana hufundishwa pia stadi mbalimbali za kazi na maisha. Lengo ni kuwawezesha vijana hao kuwa na uwezo wa kujitegemea baada ya mafunzo," alisema.

Aidha, alisema JWTZ huandikisha askari wapya kwa mujibu wa sheria, kanuni na maelekezo yanayotolewa mara kwa mara, kama ilivyofafanuliwa katika Kanuni ya Tano ya Kanuni za Majeshi ya Ulinzi, Juzuu ya Kwanza (Utawala).

"Hivyo, vijana wote wanaojiunga na JKT huandikishwa kwa kufuata utaratibu huo. Katika kipindi cha kuanzia Mwaka 2019 hadi 2022, jumla vijana 5,744 waliokuwa na sifa ikiwa ni pamoja na walioshiriki katika ujenzi wa ukuta wa Mererani , na Ikulu waliandikishwa JWTZ kwa kufuata utaratibu uliouelezea,"alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alihoji serikali haioni haja kuandikisha vijana walioshiriki kujenga Bwawa la Mwalimu Nyerere, Nyumba za Ukonga na Msomera.

Alihoji serikali ina mpango gani wa kuwa kanzidata ya vijana wanaoshiriki oparesheni maalum ili pale majeshi mengine yanapohitaji vijana wa kuwaajiri waajiriwe.

Dk. Tax akijibu swali hilo, alisema kadri nafasi zinapopatikana vijana huchukuliwa na kwamba kanzidata ipo na hushirikiana kuainisha vijana wenye sifa ya kuchukuliwa na majeshi mengine.

# Dk. Mpango ahamasisha ukuaji viwanda

**Na Joseph Mwendapole**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango ameihamasisha sekta ya viwanda nchini kuongeza mchango wake kwenye ukuaji wa pato la taifa na upatikanaji wa fedha za kigeni.

Aliyasema hayo jana wakati wa kutoa tuzo kwa mzalishaji bora wa mwaka kwenye tuzo za rais zinazotolewwa na Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI), yaani President Manufacturer of the Year Award (PMAYA).

Dk. Mpango alisema sekta ya viwanda ni chimbuko la maendeleo ya nchi na ina fursa kubwa ya kukua haraka na kutengeneza fursa za ajira na kuchochea ubunifu na maendeleo ya teknolojia.

Alisema sekta ya viwanda ni eneo muhimu la kuongeza ajira nchini na kuliongezea taifa fedha za kigeni na inamchango kwenye ukuaji wa sekta zingine kutokana na kuzalisha bidhaa zinazouzwa nje na ndani ya nchi.

"Licha ya umuhimu mkubwa wa sekya ya viwanda kwenye ukuaji wa pato la taifa, mchango wa sekta hiyo hapa nchini bado ni mdogo sana kwa hiyo wenye viwanda wanapaswa kupambana kukuza sekta hiyo.

"Nakumbuka mwaka 20021 niliwapa changamoto na leo hii narudia tena kuwataka muongeze mchango wenu katika mapato ya fedha za kigeni kwenye uchumi wetu na kwenye ajira rasmi," alisema.

Dk. Mpango alisema moja ya changamoto katika ukuaji wa viwanda ni pamoja na kushindwa kupata mikopo ya gharama nafuu, uhaba wa rasilimali watu wenye ujuzi, matumizi ya teknolojia yaliyopitwa na wakati, miundombinu hafifu na vikwazo visivyo vya kodi.

"Sasa katika kukabiliana na changamoto hizi kunahitajika jitihada za pamoja za wadau na kuongeza tija na kuongeza ushindani kwenye sekta ya viwanda mzalishe bidhaa ambazo ni nyingi na ambazo zitashindana kwenye masoko ya nje.

"Serikali inaendelea kufanya jitihada kubwa kuimarisha sekta ya uchukuzi ikiwa ni pamoja na kuimarisha usafiri wa anga, usafiri wa treni na ndiyo mara leo nimelala Dodoma na muda huu niko hapa Dar es Salaam," alisema. Dk. Mpango alisema katika jitihada za kukuza maendeleo ya viwanda serikali inaendelea kusimamia ukamilishaji wa ujenzi wa Bwawa la Umeme la Julius Nyerere (JNHPP) ambalo mpaka sasa ujenzi wake umeshafikia asilimia 99 na mitambo imeshawashwa na kuzalisha umeme.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alipongeza CTI kwa namna ambavyo imekuwa ikisimamia utoaji wa tuzo hizo tangu kaunzishwa kwake.

Rais wa CTI, Paul Makanza aliipongeza serikali ya awamu ya sita kwa namna ambavyo imekuwa ikiendelea kuwawekea mazingira mazuri wawekezaji na kusikiliza kero zao.

"Tunaomba utufikishie salamu zetu kwa mhesnimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, wawekezaji na wenye viwanda lazima tumshukuru kwa kuwa msikivu, tulikuwa na changamoto nyingi sana lakini tumekaa na serikali na nyingi zimepatiwa ufumbuzi," alisema Makanza.




Waziri wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, akizungumza katika Kongamano la kukuza ujuzi na ajira kwa vijana, lililoandaliwa na Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Tembo waliovamia kijiji warudishwa hifadhini

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

MAMLAKA ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) imefanikiwa kurudisha kwenye hifadhi makundi matatu yenye tembo 56 ambao hivi karibuni walivamia kijiji cha Mkiwa wilayani Ikungi, Singida na kuvunja nyumba nane na kula vyakula majumbani.

Ofisa Msimamizi wa Kudhibiti Wanyama Waharibifu Kanda ya Kati, Jonathan Musiba, alisema juzi kuwa tembo hao walikuwa wamejificha kwenye mapori ya vijiji vya Mkiwa, Ihanja, Mqintiri, Isuna na Gurungu.

Alisema tembo hao wamefukuzwa katika vijiji hivyo kwa kutumia ndege nyuki na kuwamwagia pilipili na kwamba sasa wamerejeshwa kwenye pori la akiba la Muhesa.

Musiba alisema mafanikio hayo yamepatikana baada ya vikosi vitatu vyenye askari 24 kutoka TAWA ambao waliweka kambi katika kijiji cha Mkiwa tangu Oktoba 28, 2024.

Hivi karibuni wananchi wa kijiji cha Mkiwa walifunga barabara kuu ya Dodoma-Singida kushinikiza serikali iwadhibiti wanyamapori wakali na waharibifu baada ya tembo kuharibu nyumba zao.

Siku moja tu baada ya wanakijiji hao kufunga barabara, Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi,Dk. Pindi Chana,alifika katika kijiji hicho na kuagiza askari wa TAWA kuweka kambi katika kijiji hicho kuwadhibi tembo hao.

Alisema hatua ya kwanza itakayochukuliwa ni kutambua mapito ya tembo ambayo yamekuwa yakitumiwa tangu enzi,kuongeza askari kwenye vijiji,kuongeza mabomu baridi yatakayotumika kusukuma wanyama hao waharibifu.

Chana alisema serikali hivi sasa inafanya sensa ya wanyapori nchi nzima ili kuangalia namna ya kuwathibiti wasiendelee kuleta madhara kwa wananchi.

Aliongeza kuwa njia nyingi inayoweza kutumika kudhibiti tembo hao ni kulima mazao kama pilipili na ufuta ambayo yanatoa harufu na hivyo inakuwa sio rahisi kwa tembo kufika kwenye mashamba na kufanya uharibifu.

Katika mkutano uliofanyika katika kijiji hicho, wananchi kwa upande wao waliomba serikali ivune tembo wakorofi ambao kila mara wamekuwa wakiharibu mashamba kubomoa nyumba na kusababisha vifo.

# Maelfu wanawake, watoto wa kike wahusishwa biashara haramu watu

**Na Beatrice Shayo**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Tanzania Relief Initiative (TRI) limesema zaidi ya asilimia 71 ya watoto wa kike na wanawake wanahusishwa katika usafirishaji haramu wa binadamu.

Mkurugenzi wa TRI, Edwin Mugambila, alisema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari na wahariri, kuhusu namna ya kuripoti matukio ya usafirishaji haramu wa binadamu yaliyofadhiliwa na Shirika la Hanns Seidel Foundation.

Alisema usafirishaji haramu wa binadamu ni uhalifu unaovuka mipaka ambao unatishia dunia kwa sasa na waathirika wakubwa ni watoto wa kike na wanawake zaidi ya asilimia 71 na maeneo yaliyoathirika zaidi ni ya vijijini.

"Maeneo yaliyoathirika zaidi ni vijijini ambapo hata taarifa hazifiki kujua viashiria vya usafirishaji wa binadamu ama ni akina nani wanaohusika na usafirishaji wa binadamu hizo taarifa huwa hazifiki hali iliyowalazimu kutoa mafunzo hayo kwa waandishi wa habari," alisema. Mugambila alisema baada ya waandishi kupata mafunzo hayo watakuwa jicho kwa jamii kwa kuibua visa hivyo vya usafirishaji haramu wa binadamu, kwa kuhabarisha jamii na kuhakikisha mitandao yote inakamatwa na jamii kubaki salama.

Mugambila alisema kwa ujumla hali sio nzuri kwa Tanzania kwa sababu imekuwa chanzo cha mapitio na mkondo wa usafirishaji haramu wa binadamu, ndio maana watoto wanasafirishwa katika sekta mbalimbali.

"Tumeona visa mbalimbali vikirepotiwa katika mashamba ya tumbaku, katika migodi, watoto wa kike wakitumikishwa katika sekta ya ngono na hivi sasa tumeona vitendo vya usafirishaji haramu wa viungo vya binadamu vimeanza kujitokeza," alisema.

Mugambila alisema watoto wanachukuliwa na kufanyishwa kazi ya ombaomba katika maeneo ya jiji la Dar es Salaam, jambo ambalo ni ukiukwaji wa haki za binadamu.

"Tanzania tuna visa vya usafirishaji wa kingono, kufanyishwa kazi za lazima, tumeshuhudia usafirishaji wa viungo, usafirishaji wa watoto ili wawe ombaomba. Hakuna nchi ambayo ipo salama katika ukanda wa Jangwa la Sahara," alisema.

Mugambila alisema Tanzania inachukua hatua stahiki na wanashirikiana na serikali kwa kutengeneza sheria imara kwa sasa na ipo taasisi ambayo inashughulikia masuala hayo.

Alisema lengo lao ni kutokomeza mtandao unaojihusisha na usafirishaji haramu na waathirika wanapatiwa ulinzi stahiki kwa mujibu wa sheria.

Alisema wanaojihusisha na biashara hiyo wanaishi katika jamii, hivyo wadau, vyombo vya habari na serikali ni lazima kuweka jicho, ili kuwatambua wote wanaohusika wafikishwe mahakamani.

Mugambila alisema sheria inaelekeza anayebainika kufanya uhalifu huo ni kifungo cha miaka 30 ama faini ya Sh. milioni 300, kutoa fidia kwa waathirika ambao wamefanyiwa vitendo hivyo.

Mwakilishi kutoka Taasisi ya Hans Seidel, Frank Gollwitzer, alisema mafunzo hayo na mada zinazotolewa kwa waandishi hao zitawapa uelewa mpana zaidi katika kupata taarifa kuhusiana na usafirishaji huo haramu wa binadamu.



Wahitimu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), wakila kiapo mbele ya Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe (hayupo pichani), wakati wa mahafali ya 59 ya chuo hicho, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Wahitimu wenye ubunifu CBE kuendelezwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) kikitarajia kusherehekea miaka 60 ya chuo hicho uongozi wa chuo hicho umesema unatarajia kuhakikisha wanafunzi wenye vipaji wanafika mbali kwa kuwa maono yao ndiyo mafanikio yao.

Mkuu wa chuo hicho, Prof. Edda Lwoga alisema hayo wakati wa hafla ya kuwatunuku vyeti na zawadi mbalimbali wanafunzi waliofanya vizuri kitaaluma kuelekea mahafali yanayotarajiwa kufanyika leo Ijumaa.

Kwenye hafla hiyo wanafunzi wa chuo hicho walionesha vipaji mbalimbali kwa kubuni vitu mbalimbali kwenye maeneo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano TEHAMA.

Prof. Lwoga alisema chuo kitafanya kila linalowezekana kuhakikisha vipaji hivyo vinaendelezwa lakini aliwasihi wahitimu kuamini katika kile wanachofanya ili kuweza kutengeneza fursa za ajira mara wanapohitimu.

"Tunafurahi kusherekea mafanikio na maendeleo ya kutimiza miaka 60 na tangu chuo kimeanzishwa kimefanikiwa kuzalisha wataalamu wa biashara na wajasiriamali pamoja na kufanikiwa kuongeza mitaala 63 kwenye ngazi za biashara, TEHAMA na metrologia," alisema.

Prof. Lwoga aliwashauri wahitimu kuendelee kujenga uwezo wa kujiajiri na kutumia teknolojia na ujuzi waliopata chuoni hapo kujiajiri na kuajiri wenzao badala ya kuhangaika kutafuta ajira kwenye kampuni mbalimbali wanapohitimu.

Naye Rais wa Sauti ya Wanawake Wajasiriamali, Maida Waziri, aliwataka wahitimu na wanafunzi walio wabunifu kusimamia ndoto zao licha ya kuwa na vikwazo katika safari ya mafanikio kwa kutoa muda na akili kwa kila wanachokifanya.

Alikiomba chuo hicho kuweka mpango wa kuwatambua na kuwaendeleza wahitimu wake waliobuni vitu mbalimbali kama alivyoona kwenye hafla hiyo kuhakikisha wanafika mbali.

"Nimetembelea maonyesho mbalimbali nimeona namna wanafunzi wenu walivyo wabunifu wa bidhaa mbalimbali kwa hiyo ninachoomba ni kwamba hakikisheni hawa wanatimiza ndoto zao, hivi vitu wanavyobuni viendelezwe," alisema.

# Maudhui ya elimu sasa kwa mtandao

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya Elimu Tanzania (TET) kwa kushirikiana na Taasisi ya Soma Kwanza Initiative, inatarajia kutekeleza mradi wa elimu kiganjani kwa kuanzisha redio, televisheni na mitandao ya kijamii, mahsusi kwa kusambaza maudhui ya elimu yaliyoandaliwa kitaalamu.

Mkurugenzi Mkuu wa TET, Dk. Aneth Komba, alisema uandaaji wa maudhui ya vipindi hivyo ambayo vitakuwa vinarushwa kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), vitazingatia mitaala ya elimu ya Tanzania.

"Katika mitaala iliyoboreshwa, serikali imeimarisha matumizi ya TEHAMA na teknolojia nyingine katika ufundishaji na ujifunzaji, ujuzi wa kidijitali ambayo ni mojawapo ya stadi muhimu za karne ya 21, zimebainishwa bayana katika malengo makuu ya elimu nchini, hivyo programu hizo zitawekwa katika vitendo vya ufundishaji na ujifunzaji kwa masomo yote kuanzia ngazi ya elimu ya awali.

"Makubaliano ambayo tumeyasaini leo(jana), yamekuja wakati mwafaka wakati serikali inaendela kuimarisha matumizi ya Tehama katika ufundishajia na ujifunzaji," alisema Dk. Komba.

Alisema katika makubaliano yao baadhi ya majukumu ya TET yatakuwa kuratibu utekelezaji wa mradi kuhakikisha unafanyika kwa mujibu wa sera ya elimu ya nchi, kutoa nyaraka za mitaala na muhtasari, kushiriki katika uaandaaji wa maudhui ya kidigitali na kuidhinisha maudhui ya kidigitali yatakayoandaliwa.

"Tutakuwa tunaongoza na kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa kushirikiana na wadau wengine wanaohusika, kuandaa TET Soma Kwanza TV, Soma Kwanza Radio, na Soma Kwanza App na kutumia vyombo hivyo kwa ajili ya kusambaza taarifa za elimu," alisema Dk. Komba.

"Baadhi ya majukumu ya Soma Kwanza initiative ni kutoa fedha za kutosha kwa ajili ya utekelezaji mradi huu, kuwezesha ufuatiliaji na tathmini, kushirikiana na TET kuandaa maudhui ya elimu ya kidijitali na kusimamia utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya miradi.

"Lengo na fahari yetu sote ni kuona mradi huu unafikia mafanikio yanayotarajiwa na kuchangia katika utekelezaji wa mitaala iliyoboreshwa," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Soma Kwanza, Peter Kangere, alisema wamefikia makubaliano hayo ya kuanzisha televisheni, radio pamoja na kusambaza maudhui mitandaoni mahsusi ya kutoka elimu kiteknolojia, baada ya kufanya utafiti kwa miaka minnne.

"Lengo kubwa ni kuwawezesha watoto kutoka katika familia zote bila kujali hali zao za kijamii na kiuchumi, kupata maudhui bora ya kielimu ya kusaidia kufikia hatma ya maisha.Dunia inazidi kuwa ya kidijitali kwa kutumia Tehama, tunataka kuhakikisha hawabaki nyuma katika mabadiliko haya.

"Kama ilivyo dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kutoa elimu bora na iliyo sawa kwa watoto wetu, hatua hii inalenga kuendeleza juhudi hizo za serikali kwa kutumia teknolojia na tunataka maudhui ya elimu yatakayosambazwa yawiane na mitaala ya Tanzania ili wanafunzi wa mijini na vijijini wapate elimu bora na kwa njia rahisi," alisema.



## Samia kuzindua mfuko wa mikopo ubunifu, teknolojia

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, Desemba 2, mwaka huu, anatarajiwa kuzindua mfuko wa mikopo kwa ajili ya kusaidia ubidhaishaji na ubiasharishaji wa ubunifu na teknolojia zinazobuniwa na vijana wa kitanzania.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Aldolf Mkenda, alibainisha hayo juzi wakati akitambulisha kongamano la tisa la kitaifa la Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (STICE), linaloratibiwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH).

Prof. Mkenda alisema katika kongamano hilo lililopangwa kufanyika Desemba 2 hadi 4, mwaka huu katika Ukumbi wa Kimataifa wa Mikutano wa Julius Nyerere (JNICC), Dar es salaam.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na kuzindua mfuko huo, atakabidhi hundi yenye thamani ya Sh. bilioni 6.3 kwa watafiti 19 katika masuala ya mabadiliko ya tabia nchi ikiwamo nishati safi ya kupikia.

Alisema Rais Samia pia atawatambua na kutoa tuzo maalum kwa wanasayansi na wabunifu ambao matokeo ya kazi yao yamechangia kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii ndani na nje ya nchi.

Prof. Mkenda alisema kaulimbiu ya kongamano hilo ni matumizi ya sayansi, teknolohia na ubunifu katika kuhimili mabadiliko ya tabianchi na kuchangia kwenye uchumi shindani.

Alisema ni imani yake kuwa kupitia kongamano hilo serikali itapata michango ya kisera na kitaaluma ambayo itasaidia kuimarisha sera mikakati na juhudi nyingine zinazolenga kuimarisha mchango na mshikamano baina ya taasisi, sekta binafsi na wadau wamaendeleo.

Aidha, Prof. Mkenda aliishukuru timu nzima ya maandalizi ya kongamano hilo na kuongeza kuwa STICE ya mwaka huu itakuwa ni hatua nyingine muhimu katika safari ya kujenga taifa linaloongozwa na sayansi, teknolojia na ubunifu.

Mkurugenzi Mkuu wa COSTECH, Dk. Amos Nungu, alisema lengo la kongamano hilo ni kuwakutanisha wadau mbalimbali kujadili mambo mbalimbali yanayohusu sayansi na teknolojia ikiwemo kuonyesha mambo wanayoyafanya wabunifu.

Dk. Nungu alisema, Oktoba 4, mwaka huu, walizindua mwongozo wa kitaifa wa masuala ya ubunifu ili uweze kufikiwa na kusaidia kila aina ya ubunifu unaofanywa na wabunifu.

Alisema muongozo huo pia una mtaala mpya ambao utawasaidia wanafunzi wenye vipaji kwanzia ngazi ya chini ambao watapata

# RC aonya wanaolaghai wanafunzi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
ITIGI

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, ameonya kuwa hataki kuona mtu yeyote anacheza na wanafunzi wa kike wanapokuwa ndani na nje ya shule.

Amesema wanafunzi hao wanapaswa kuheshimiwa ili kuzifikia ndoto zao za maisha na kuwawezesha kusoma katika mazingira bora na rafiki.

Dengego alitoa onyo hilo juzi katika Shule ya Sekondari Kitaraka, Halmashauri ya Itigi, alipokuwa akikagua mradi wa ujenzi wa nyumba ya mwalimu (Two in One) ambayo yamejengwa kupitia Programu ya Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP).

Alisema licha ya kuwa serikali na jamii inatumia nguvu kubwa kuwalinda watoto wa kike dhidi ya ulaghai unaoweza kusababisha ndoto zao kuharibika, ni wajibu wao wanafunzi kuhakikisha wanajilinda kwa kujiheshimu na kujiweka mbali na ushawishi wa wale ambao wanaonyesha dalili mbaya dhidi yao.

Wanafunzi hao, alisema lazima watambue kuwa ikiwa watapata ujauzito wakiwa katika masomo ni wazi kuwa nao wameshiriki katika kujiweka katika matatizo, hivyo watawajibika na si upande wa mwanamume pekee.

"Wanafunzi ni nyara za serikali zenye gharama kubwa sana ndio sababu serikali ikaweka sheria ya miaka thelathini jela kwa watakaokuka na kuwalaghai watoto wa kike,tutawalinda siku zote mchana na usiku," alisema.

**"Watoto wasio na 'uniform' (sare) wasifukuzwe darasani. Tunachotaka watoto wapate elimu na katika mkoa wa Singida kwa sasa tuna operesheni ya kutokomeza matokeo ya daraja...**

Mkuu wa Mkoa pia aliagiza watoto wapewe kipaumbele katika kusoma kwa kushiriki masomo darasani na wenzao hata kwa wale ambao hawana sare za shule wasirudishwe nyumbani bali wapewe nafasi huku wakiendelea kuwa na utayari.

"Watoto wasio na 'uniform' (sare) wasifukuzwe darasani. Tunachotaka watoto wapate elimu na katika mkoa wa Singida kwa sasa tuna operesheni ya kutokomeza matokeo ya daraja la nne na daraja ziro," alisema.

Sambamba na hilo, alisisitiza utunzwaji mzuri wa nyumba hizo za walimu kwa kupanda miti maeneo yote yanayozunguka shule eneo hilo kwa lengo la kutunza mazingira lakini pia kujipatia kipato kutokana na miti kama aina ya mikorosho. Aliagiza upatikanaji wa bendera ya taifa shuleni hapo itakayotumika wakati wa kuimba wimbo wa taifa na kuwekwa kwa mfumo wa kuvuna maji ya mvua ili kupunguza kero ya uhaba wa maji shuleni hapo.

Dedengo pia aliahidi kuongezwa kwa walimu wa masomo ya Fizikia, Kemia na Hisabati kwa lengo la kutatua ukosefu wa walimu wa masomo hayo shuleni hapo na kuagiza kuwapo na mlinzi wa shule ambaye amepitia mafunzo kwa uhakika wa usalama wa mali za shuleni hapo.

Naye Mkuu wa Shule ya Sekondari Kitaraka, Amani Mwamakula, aliishukru serikali kwa kuwapatia fedha hizo za kujenga nyumba ya mwalimu kwa kuwa itaboresha mazingira ya utoaji elimu kwa wanafunzi na ulinzi wa mali za shule na walimu wataondokana na kutembea umbali mrefu kufika shuleni.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kushoto), akiagana na Wabunge, baada ya kuahirisha shughuli za mkutano wa 17 wa Bunge hadi Januari 28, 2025, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali yafuta leseni 2,649 uchimbaji madini

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI imefuta leseni za uchimbaji na kuondoa maombi 2,648 ambayo hayajakidhi vigezo na kuyarudisha serikalini ili kuwapatia wanawake na vijana kwa ajili ya uchimbaji madini na kujiinua kiuchumi.

Waziri wa Madini, Antony Mavunde, alisema hayo wakati akifunga kongamano la Jukwaa la Uziduaji Tanzania, lililofanyika jijini hapa, chini ya uratibu wa Asasi 16 za kiraia (HakiRasilimali).

Mavunde alisema uondoaji wa leseni hizo na maombi hayo umefanyika baada ya kupata maelekezo kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwamba wahakikishe leseni zote na maombi ambayo hayajakidhi vigezo na sifa yanaondolewa.

Alisema tayari wameanza kufanya kazi hiyo ili maeneo hayo yatolewe kwa wanawake na vijana kwa ajili ya kuendelea na uchimbaji madini kama walivyokusudia.

"Serikali imekwishachukua hatua kwenye hilo tayari tumefuta leseni na kuondoa maombi ambayo hayajakidhi vigezo zoezi hilo bado linaendelea, sekta ya madini inahitaji watu waaminifu," alisisitiza Mavunde.

Alisema wako Watanzania 12 ambao walikuwa wanamilikimaeneo ya uchimbaji madini yenye ukubwa wa ekari 4,300,000 huku wengine 34 ambao waliingiza maombi ya ekari 13,400,000 hali ambayo wanashindwa kuyafanyia kazi na kuwakosesha watu fursa za kufanya shughuli za madini.

"Serikali haiwezi kuvumilia suala hilo ndiyo maana tunaendelea kuondoa maombi yasiyokidhi vigezo ikiwemo kufuta leseni," alisema.

Mavunde alisema HakiRasilimali imekuwa na mchango mkubwa katika kuboresha sera, sheria na mipango katika sekta ya uziduaji, hivyo asasi hiyo ni muhimu kwa serikali kwa sababu inachangia kukuza sekta ya uziduaji nchini.

Alisema HakiRasilimali si maadui wa serikali isipokuwa ni watumuhimu ambao wanaisaidia serikali ili kuhakikisha sekta ya uziduaji Tanzania inazidi kupiga hatua na kusaidia jamii kujiinua kiuchumi kupitia sekta hiyo.

Mavunde alisema katika maazimio tisa waliyoyatoa, serikali imeyachukua na kuahidi kwenda kuyafanyia kazi ili sekta hiyo izidi kuboreshwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Kuhusu matumizi ya zebaki, Mavunde alisema serikali kupitia Shirika la Madini Tanzania (STAMICO) imeanzisha vituo vya mafunzo katika maeneo ya Chunya na mengine vya kuwasaidia kuwabadilisha kimtazamo wachimbaji wadogo ikiwemo kuwajengea uwezo wachimbaji hao kutoka kwenye matumizi ya zebaki kwenda kutumia mitambo midogo ambayo inarahisisha kukamata dhahabu.

Mkurugenzi Mtendaji wa HakiRasilimali, Adam Antony, alisema baadhi ya maazimio waliofikia katika Jukwaa hilo ni pamoja nakuhimiza serikali kutenga maeneo maalum kwa wanawake wanaojishughulisha na uchimbaji wa madini ili kuwawezesha na kuwahamasisha kufanya kazi hiyo. 00Alisema hatua hiyo itasaidia kupunguza changamoto wanazokutana nazo wanawake kama unyanyasaji wa kijinsia unaotokana na imani potofu.



## Watakiwa kufundisha wanafunzi kidijitali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Khamis Abdallah Said amewataka walimu kufundisha kidijitali shuleni ili watoto waende sambamba na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Abdallah aliyasema hayo wakati akikabidhiwa chumba cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kupitia Mradi wa Kuboresha Huduma za Maabara za TEHAMA (EQSSE-Z) kwa Shule za Unguja na Pemba.

Alisema serikali inafanya mageuzi makubwa ya elimu kwa kutumia TEHAMA katika shule mbalimbali Unguja na Pemba na kujenga maabara za kisasa lengo ni kuona watoto wanajifunza kivitendo zaidi.

Alisema serikali kupitia bajeti ya wizara ya elimu imetenga jumla ya Sh. bilioni 12 kwa ajili ya idara ya mafunzo kazini ambapo fedha nyingi zitatumika kuwapa mafunzo walimu. Aliwataka walimu kuhakikisha wanasimamia jukumu lao la kufundisha kwa bidii watoto ili kuendelea kufanya vizuri katika masomo yao.

Kadhalika aliahidi kuendelea kuweka mazingira mazuri katika vyumba vya TEHAMA ili kuhakikisha walimu na wanafunzi wanatumia wakati wote.

Katibu Khamis aliwataka walimu wakuu kushirikiana na ofisi za elimu wilaya na mikoa kuhakikisha wanasimamia walimu kufundisha watoto ili Zanzibar iendelea kupata matokeo mazuri ya elimu.

Alisema hivi sasa kumekuwa na ongezeko la ufaulu kwa wanafunzi hasa katika masomo ya sayansi kutokana na jitihada zinazochukuliwa na serikali, walimu na wadau wengine wa maendeleo.

"Ushirikiano wetu kwa pamoja katika kuwahudumia watoto wetu ndio utakaotuwezesha kupata taifa bora," alisema.

Aliwataka wasimamizi wa vituo hivyo kuhakikisha wanavitunza vifaa vilivyokuwapo katika vyumba hivyo na kuvitumika vizuri kama ilivyokusudiwa.

Meneja wa Mradi wa Kuboresha Elimu kutoka Good Neighbars Tanzania, Ye Jincho, alisema kutokana na kukua kwa teknolojia ya ufunzaji na ufundishaji, mradi huo uliona kuna haja ya kusaidia katika vifaa vya TEHAMA katika vituo vya walimu vitano kwa Unguja na Pemba.

Alisema lengo la kusaidia vifaa hivyo ni kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika shughuli za ufundishaji na ufunzaji.

Alisema anaamini makundi mbalimbali yatatumia vituo hivyo katika kurahisisha ufundishaji na ufunzaji kwa watoto wao.

Alisema vifaa hivyo ikiwamo kompyuta 155 vitasaidia kunufaisha walimu na wanafunzi katika matumizi ya TEHAMAnchini.

Mkurugenzi wa mafunzo ya ualimu anayeshighulikia TC Unguja na Pemba, Othman Omar Othman, aliipongeza Good Neighbors kupitia KOICA kujitoa kwao kuhakikisha lengo kuu la ubora wa elimu linafikiwa ikiwamo kutoa mafunzo kwa walimu wa shule za sekondari.

Alisema mafunzo ya ualimu yamesaidia kupata walimu wanaofundisha katika viwango vilivyobora na kupata wanafunzi ambao watakuwa wataalamu na wataendeleza taifa lao baadaye. Wasimamizi wa vituo hivyo waliahidi kuvitunza vituo hivyo na kuhakikisha vinatumika vizuri kama ilivyokusudiwa ili wanafunzi kufanya vizuri hasa katika mitihani yao ya taifa.

# Wahadharishwa utapeli ajira vikosi SMZ

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Massoud Ali Muhammed amewataka wananchi wasikubali kutapeliwa kwa madai ya kupatiwa ajira za Vikosi vya SMZ.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari, Waziri huyo alisema serikali imeweka mfumo mzuri wa kuajiri na kuwatahadharisha wananchi kutokubali kutapeliwa kwa madai ya kupatiwa ajira.

Alisema serikali haitomfumbia macho mtu yeyote atakayebainika kufanya utapeli huo na kuwataka wananchi kuwaripoti watakaowabaini kufanya vitendo hivyo, ili kuchukuliwa hatua za kisheria.

Alisema jumla miradi 64 imetekelezwa kwa kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Waziri huyo alisema licha idara maalum kutekeleza jukumu la msingi la kulinda amani na utulivu, lakini imeshiriki katika ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo masoko, elimu na uchumi wa buluu.

Alisema baada ya kukamilisha ujenzi wa miradi ya barabara, serikali inakusudia kuanzisha mradi maalum wa usafi, utakaotumia vitendea kazi vya kisasa. Alisema serikali imetumia fedha nyinyi kwa ajili ya ujenzi wa masoko, hivyo haitomfumbia macho mtu atayefanyabiashara katika maeneo yasioruhusiwa yakiwamo barabarani.



Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ya Baraza la Wawakilishi, Mwanaasha Khamis (katikati), akiongoza kikao cha kupitia ripoti ya utekelezaji wa mradi wa elimu ya juu kwa mabadiliko ya kiuchumi (HEET), katika Chuo cha Taifa Zanzibar (SUZA), Tunguu, nje ya mji wa Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wadadisi wa utafiti kilimo wahimizwa kutilia mkazo mafunzo wanayopatiwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MTAKWIMU Mkuu wa Serikali, Salum Kassim Ali, amewataka wadadisi wa utafiti wa kilimo kuzingatia kwa makini mafunzo wanayopatiwa ili kuifanya kazi hiyo kwa ufanisi.

Salum aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya wadadisi wa utafiti wa kilimo kwa mwaka 2023/2024 katika ofisi za Mtakwimu Mkuu wa Serikali (OCGS), Mazizini.

Alisema utafiti huo unahitajika katika kufuatilia na kutathmini malengo yaliyowekwa katika sera na mipango ya maendeleo ya kuendeleza sekta za kilimo, mifugo na uvuvi.

Alisema kwa mujibu wa Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO), kilimo ndiyo sekta kubwa inayochangia pato la Afrika kwa asilimia 15 ya sekta zote au zaidi ya dola za Marekani bilioni 100 kwa mwaka.

"Ni dhahiri kuwa kilimo kinatumika kwa asilimia 100 kulisha watu bilioni 1.47 katika Bara la Afrika na kuchangia uchumi wa Afrika kwa asilimia 15.

"Kwa msingi huo katika Bara la Afrika, Ofisi za Taifa za Takwimu kama vile NBS na OCGS zimeendelea kutoa kipaumbile katika kuimarisha uzalishaji wa takwimu za kilimo, mifugo na uvuvi kwa lengo la kuimarisha utungaji sera zinazohusu sekta hizo", alisema Salum.

Alisema kutokana na maendeleo ya teknolojia, utafiti huo utafanyika kisayansi kwa kutumia teknolojia ya kisasa ambayo itapunguza gharama za kukusanya na kuchakata takwimu hizo kwa kiasi kikubwa.

Aliwakata wananchi kutoa ushirikiano wa kutosha wakati wadadisi watakapofika katika maeneo yao kukusanya taarifa hizo.

"Ikumbukwe kuwa taarifa sahihi zitakapotolewa ndiyo msingi nwa serikali kupanga mipango sahihi kwa ajili maendeleo ya sekta za kilimo, mifugo na uvuvi.

Wadadisi waliopatiwa mafunzo hayo, waliahidi kuyafanyia kazi kwa uadilifu na weledi kwa kufuata sheria na taratibu bila ya kutoa siri.



FERUZ

UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE





# WAKAZI ASISIKIE KITU, friji lake haligandishi

RAPA maarufu, Wakazi, anajulikana na wengi kutokana na tabia yake ya kuibua matukio mengi yanayosababisha mitafaruku kati yake na wasanii wenzake.

Hivi karibuni msanii huyo alikuwa na majibizano makali na mwimbaji Zuchu, kiasi ambacho wanamuziki hao walifikia hatua ya kutoleana siri za ndani za matukio ya zamani.

Sio kwa Zuchu tu, Wakazi amewakosoa wasanii mbalimbali na wakati mwingine kuingia katika majibizano makali.

Kimsingi huyo ndiye Wakazi, ambaye licha ya kupata umaarufu katika muziki wa Hiphop, amepandisha jina lake kwa mijadala tata anayoibua kupitia kurasa zake za mitandao ya kijamii.

Kutokana na tabia yake ya ukosoaji wa wazi, wapo wanaomuona kama shujaa, lakini wengine wanapingana naye kwa kumfananisha na mtu anayetaka umaarufu kupitia majina ya watu.

Wanaokubaliana naye wanaeleza kwamba amekuwa alama ya kutokubaliana na kile kinachoendelea katika maisha ya wasanii wengi.

Wanasema wanamuziki wengi wa Bongo Fleva, wanaishi katika mazingira feki tofauti na mashabiki wao wanavyofahamu. Lakini kwa kupitia Wakazi wanajua hali halisi inayowazunguka.

Wakosoaji wake, wanaamini kwamba hakuna umuhimu kwa wasanii wakubwa kukosoana hadharani na kusababisha mitafaruku.

Wanasema njia anayoitumia haileti afya katika tasnia ya muziki na badala yake inajenga chuki, ugomvi na kutokuaminiana.

## BASI SAWA

## Ferouz hana ugomvi na Chino



MWANAMUZIKI Mkongwe Ferouz amesema hana ugomvi na Chino, licha ya kupelekana katika vyombo vya sheria kutokana na kazi zao za muziki.

Amesema kwa sasa wao wawili hawana matatizo baada ya Chino kulipa kiasi kidogo cha pesa baada ya kutumia kazi yake bila ruhusa.

"Mimi na Chino hatuna matatizo, sisi ni wasanii wa muziki tunaweza kufanya kazi wakati wowote. Nilimshtaki kwa sababu nilitaka wasanii wengine chipukizi kujua ubaya wa kutumia kazi za wengine bila ruhusa," amesema Ferouz.

## Msechu kapenda hatari



MWANAMUZIKI Peter Msechu, amesema kila anachotaka kufanya lazima anamshirikisha mke wake kwa kuwa ndiye mtu maalumu kwake.

Akizungumzia biashara yake ya samaki, amesema yeye na mke wake wanatoka Mkoani Kigoma, hivyo kwa pamoja waliamua kuanzisha biashara hiyo ambayo kwa sasa imeanza kuleta mafanikio.

"Mimi na mke wangu tulikuwa tunapata tabu kupata samaki wa Migebuka kutoka Kigoma, hapo ndipo kwa pamoja tuliona kama fursa kuanza kuagiza kutoka Kigoma kwa ajili ya biashara," amesema Msechu.



## MSIKIENI SHILOLE ANACHOSEMA

MWANAMUZIKI na mjasiriamali, Shilole, amewaasa watu wanaosaka mafanikio kuhakikisha wanakuwa na bidii kutimiza ndoto zao.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Shilole, amesema jambo la kuzingatia ni kutumia kila pesa kwa malengo kwa sababu huleta thamani ya kweli kwenye mafanikio.

"Kila shilingi unayoipata ni matokeo ya bidii na maarifa yako, Ithamini sana pesa yako, usiache kusali, Mungu atasikia kilio chako hiyo riziki unayoipata iongezeke mara dufu, ameandika Shilole.



## Itslouiagain kwake ni tofauti

MSANII chipukizi wa Bongo Fleva, Itslouiagain, amesema hasira za kutafuta jina katika muziki ilimfanya kupita njia ambayo wengi wanashindwa.

Akizungumza hivi karibuni, Itslouiagain amesema mara nyingi huwa anafanya tofauti na wanamuziki wengine ikiwa ni pamoja na nyimbo zake nyingi kuimba kwa lugha ya kiingereza tofauti na wengine.

"Nilianza kuwa tofauti tangu nilipokuwa naingia kwenye fani, nakumbuka siku moja Ney wa Mitego aliniambia niimbe kwa Kiswahili ili kupata mashabiki wengi, nilichukua ushauri wake kwa mtazamo hasi na kuandika wimbo Kiingereza ambao unapendwa hadi sasa," amesema.

## ZIMEBAMBA KINOMA OKTOBA

**Na Adam Fungamwango**

UMEINGIA mwezi Novemba, ukichukua nafasi ya Oktoba ambao umeondoka zake. Watakaobarikiwa watauona mwakani tena.

Umeondoka na kuacha rekodi ya ngoma kali kurekodiwa mwezi huo. Wasanii kibao wakubwa wakubwa wametoa ngoma zao ambazo zimebamba na kuwatikisa mashabiki wa muziki wa bongo fleva.

Tuzitazame ngoma tano kali ambazo zimefyatuliwa mwezi Oktoba na zinaendelea 'kutrendi' kwenye mitandao mbalimbali ya kijamii, redio na televisheni.

### Attention-Whozu ft Zuchu

Siku nne tu baada ya kuingia mwezi Oktoba, msanii Whozu awahi bwana. Akafyatua ngoma yake mpya akaiita 'Attention.' katika wimbo huu akamshirikisha bibie, Zuchu na kuufanya uchangamke kinoma.

Kwenye akaunti ya msanii huo ndani ya mtandao wa 'you tube', wiki hii ulikuwa umekamata nafasi ya tisa kwa kuangaliwa na watu wengi zaidi.

### Natamba Naye-Phina

Msanii wa kike wa bongo fleva, Phina, yeye akaja na ngoma yake iitwayo 'Natamba Naye', Oktoba 11 na kuwa mwanamke wa kwanza kutoa ngoma mwa mwezi huo.

Kama kawaida ni wimbo wa mapenzi, ambao wameanza kuwa gumzo kwa mashabiki wa muziki huo.

### Usemi Sina- Nandy ft Harmonize

Hapa katikati kama vile kulilegea, lakini mwishoni wa Oktoba, moto uliwaka pale, mwanadada Nandy naye alipoamua kuja na pini lake lake liitwalo 'Usemi Sina.' Katika kulinogesha, akamshirikina na mmoja wa wasanii nyota nchini Tanzania, Harmonize, maarufu kama Tembo. Kwa taarifa tu, ni kwamba ngoma hii iliyofyatuliwa Oktoba 24, inakamata nafasi ya pili kwa kuangaliwa zaidi kwenye mtandao wa 'you tube' katika akaunti ya mwenyewe, Nandy.

### Sir God-Chege ft D Voice & Billnass

Siku moja baada ya Nandy kuporomosha ngoma hiyo, msanii wa siku nyingi nchini, Chege, naye akafyatua ngoma mpya inayoitwa 'Sir God.' Ndani ya ngoma hiyo kuna mchanganyiko wa vionjo, kwani Chege akishirikisha damu changa kama D Voice, halafu akamuweka na Billnass kwenye ngoma hiyo.

Tangu ilipotoka Oktoba 25 inashuka nafasi ya 16 kwa 'kutrendi' kwenye akaunti yake kwenye mtandao wa 'you tube.'

### Itakuwaje-Barnaba

Oktoba 30, msanii Barnaba naye akamaliza kwa ngoma yake 'Itakuwaje.' Msanii huyo analalamika juu ya mapenzi wake ambao kwa sasa hayupo naye, akikumbuka yote ambayo ambayo waliyokuwa wakiyafanya wakati wakianza mapenzi yao kwa tabu sana. Akakumbuka yote ambayo mkewe alivyokuwa akimfanyia. Kwa sasa mke ameondoka kwa sababu amemfumania na amepigwa kweli kweli hasi kutembea hawezi. Anatembea na magongo, hakuna wa kumsaidia ale nini.



## FILAMU

# Binti Albino: Nitakulinda

**Na Adam Fungamwango**

BINTI Albino ni filamu kali, yenye msisimko, mafunzo na ya kusikitisha, inayosimulia juu ya watu wanaotaka utajiri wasioufanyia kazi kwa kuwaua, na kukata viungo vya watu wenye ulemavu wa ngozi, wakidanganywa na baadhi ya waganga kuwa vinaleta utajiri, au vyeo.

Filamu hii imetengenezwa kwa simulizi kutoka baadhi ya watu wenye ulemavu wa ngozi kuhusu visa na mikasa iliyowakuta kwa sababu ya kuwa na hali hiyo.

Miaka 25 iliyopita baba na mama mmoja kwenye moja kati ya vijiji vya Tanzania, walimzaa mtoto wao waliyemwita Sam. Ni mtoto Albino. Malezi yake yalikuwa ya tabu, kwani wazazi hao walipata tabu ya kumlea na kumlinda kutokana na hali yake hiyo.

Mara kwa mara baadhi ya watu wabaya, wakishirikiana na waganga feki, walikuwa wanamuwinda ili wamuue kwa ajili ya kuchukua viungo vyake.

Siku moja walivunjiwa mlango na watu waliokuwa wanataka kuchukua roho ya mtoto na kwa bahati nzuri, mama na mtoto walitoka kidogo. Baba waliyemkuta walimpiga na kumuacha akitapatapa.

Mke aliporejea alimkuta mumewe kwenye hali mbaya. Akamwambia mkewe amevamiwa na watu waliomtaka mtoto, hivyo amkimbize haraka kwa babu yake. Mke akafanya hivyo. Huku nyuma mume alifariki. Mke aliporejea naye alikutana na watu hao, akauawa.

Sam aliishi kwa babu yake na alipofikisha umri wa miaka 25, babu yake aliamua kumwambia ukweli wote.

Akapatwa na hasira na kusema anataka kulipiza kisasi kwa wote waliouwa wazazi wake, na wanaosaka viungo vya Albino kwa madai ya kutaka kujipatia utajiri.

Babu alimzuia. Akamwambia hata kama anataka kulipiza lakini hawezi, kwa sababu bado hajaiva kwenye kila kitu.

Kesho yake akiwa porini aliwasikia watu ambao walikuwa wamefika kwenye kijiji hicho kwa ajili ya kuwasaka Albino baada ya kuagizwa na waganga wa kienyeji.

Akarudi mbio na kumwambia babu yake. Babu kuona hivyo, akaanza kumfundisha mjukuu wake, kulenga shabaha kwa kutumia mishale, pamoja na kumtengeneza kuwa na utimamu wa mwili.

Baada ya kuhakikisha ameiva, akamwambia sasa anaweza kupambana na mtu yoyote ikiwemo kwa waliotaka kumuua na na hata kulipiza kisasi cha walioua wazazi wake. Anamkabidhi upinde mishale.

Mzee mmoja jirani naye alikuwa na watoto wawili Albino, mmoja kijana na mwingine binti. Sam akawafuata na kuwaambia atahakikisha anawalinda. Akwambia binti kuwa atamlinda kama malkia.

Kilichotokea ni historia, kwani Sam aliteketeza kundi lote hatari lililokuwa linaua Albino. Aliwateketeza waliomuua baba na mama yake, waliokuwa wanalipwa pesa kusaka Albino, waganga wa kienyeji na hata wale waliokuwa wakisaka utajiri. Alikuwa akitumia ngumi, kareti na upende na mishale. Kijiji kikarudi kwenye hali ya amani na utulivu.



# Vector awashangaa Waafrika

UCHAGUZI wa Marekani umemuibua rapa mkali wa Nigeria, Vector ambaye ameonesha kushangazwa kwake jinsi waafrika walivyoshabikia uchaguzi wa rais wa Marekani.

Rapa huyo alitumia ukurasa wake wa X kwa kueleza maoni yake kwamba hajawahi kuwaelewa Waafrika kwa kuweka mshikamano katika mchakato huo jambo ambalo katika nchi zao hawafanyi hivyo.

"Sijawahi kuwaelewa Waafrika ambao wanaonesha aina fulani ya mshikamano na mchakato wa uchaguzi katika mataifa ambayo yanatushinda sote kwa riziki." Ameandika.





## Ufoma atoa ushauri mzito

MWIGIZAJI wa Nigeria, Ufoma McDermott amefunguka kuhusu ugonjwa wa figo unaomsumbua, akisema unatokana na muda mrefu wa matumizi ya dawa za maumivu.

Ufoma ambaye ni mwigizaji kutoka Nollywood, alisema anapitia kipindi kigumu kwa miaka 12 akipambana na matatizo ya figo, yote yanatokana na kutozingatia utaratibu mzuri wa kutumia dawa.


"Natamani sana kila mtu angeelewa umuhimu wa afya, kaka yangu alichelewa kufika hatua ya nne ikabidi aingie kwenye mashine moja kwa moja na kupata matatizo, mimi niligundulika mapema sana hivyo nimeishi kwa kutumia dawa kwa karibu miaka 12 sasa." Amesema

## Halle Bailey atibuliwa

MWIMBAJI na mwigizaji wa Marekani, Halle Bailey, amekasirishwa na kitendo cha mpenzi wake wa zamani DDG, kumchukua mtoto bila idhini yake.

DDG wiki iliyopita alionekana akiwa na mtoto wake Halo, wakati akiwa katika kipindi kimoja cha televisheni.

"Mimi niko nje ya mji na sijaidhinisha mtoto wangu achukuliwe na baba yake. Sikuambiwa au kuarifiwa na nimekasirika sana mtoto wangu kuwa mbele ya mamilioni ya watu." Amesema.





## Angel atangaza kuwa singo

BAADA ya kuwepo kwa tetesi kwa miezi kadhaa, sasa nyota wa BBNaija, Angel, amethibitisha kuwa uhusiano wake na aliyekuwa mchumba wake Soma umefikia kikomo.

Akizungumza hivi karibuni kupitia ukurasa wake wa X, amesema wameamua kuwa mbali kutokana na kuwa na mapenzi yaliyogawanyika baaada ya kugundua Soma anajihusisha na mpenzi wake wa zamani Hilda.


"Taratibu nimejitenga na kila kitu kilichotokea, siwezi kushambulia mtu. Kama nilivyosema, niko katika nafasi nzuri ya kiakili, niko kwenye mazoezi, na sitaki chochote cha kunisumbua. Nilichanganyikiwa tu kwa nini ex wake alikuwa akinitukana," amesema .

## Tabasamu la Ckay hatarii

MWANAMUZIKI wa Nigeria, CKay ameeleza wanawake wengi wanapenda tabasamu lake na wakati huonesha furaha yao kila wanapomuona.

Amesema wakati mwingine wanamshauri kuongeza tabasamu, lakini kwake huona hakuna umuhimu kwa sababu ndivyo alivyoumbwa na Mungu.

"Mara kwa mara huniambia nina tabasamu zuri na ninapaswa kutabasamu zaidi, kama vile sitabasamu vya kutosha. Sijui, jamani; labda sitabasamu vya kutosha. katika picha. Nadhani ndivyo ilivyo kwa sababu watu huniona kwenye picha nyingi zaidi kuliko mimi ninavyojiona katika maisha halisi," amesema huku akitabasamu.





# Kesi ya mwekezaji yapigwa kalenda

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

KESI ya uhujumu uchumi, inayomkabili mfanyabiashara na mwekezaji, Saleh Alamry (54), imepigwa kalenda baada ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha kuelezwa na upande wa mashtaka kuwa upelelezi utakamilika ndani ya siku saba zijazo.

Jana, katika mahakama hiyo iliyoko Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki-Arusha, Wakili wa Serikali, Ahmed Mbagwa, aliieleza mahakama hiyo kuwa kutokana na jitihada wanazoendelea kuzifanya, wanatarajia kukamilisha upelelezi ndani ya wiki moja.

Kesi hiyo inayovuta hisia za wakazi wa mikoa ya Kaskazini, inasikilizwa na Hakimu Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Erasto Philly. Aidha, Wakili wa Utetezi, Feisal Rukaka, aliiomba mahakama hiyo kutenda haki kwa mteja wao, huku wakiomba mahakama kutoa maelekezo kwa Jamhuri kukamilisha upelelezi wao kwa muda walioomba.

Baada ya maelezo hayo ya upande wa mashtaka, Hakimu Philly, alisema mahakama hiyo inakubaliana na maombi ya pande zote mbili. Huku, akiitaka Jamhuri kutoifanya mahakama kama kichaka cha kujifichia, kwa kupoteza muda wa kutokupeleka ushahidi ili mshtakiwa mmoja kati ya wawili aendelee kuteseka rumande.

Hakimu Philly alisema shauri lililoko mahakamani hapo linatakiwa kusikilizwa na mahakama kuu, hivyo upelelezi huo utakapokamilika, itaamua kutoa kibali cha mahakama hiyo kuendelea kuisikiliza au la.

Kesi hiyo imehairishwa hadi Novemba 21 mwaka huu, itakapotajwa tena.



Mpima Ardhi wa mkoa wa Tanga, Shaban Mruma (kulia), akitoa maelezo ya tafsiri ya mpaka wa Wilaya ya Handeni na Pangani, kwa viongozi wa vijiji vya Mtonga wilayani Handeni, mapema wiki hii, ili kutatua mgogoro wa mipaka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wageni 500 Afrika watembelea Ngorongoro

**Na Godfrey Mushi,** NGORONGORO

ZAIDI ya wageni 500 kutoka sekta ya umma katika mataifa mbalimbali Afrika, wamelitembelea eneo la Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), kujionea urithi wa dunia na vivutio adimu vya kitalii vilivyoko Tanzania, wakiwemo wanyama watano wakubwa.

Waliotembelea eneo hilo la Ngorongoro ni mameneja wa rasilimali watu katika sekta ya umma Afrika, wakiongozwa na Rais wa Mtandao huo (APS-HRMNet), Xavier Daud.

Kwa mujibu wa Rais huyo APS-HRMNet, mameneja hao wamepata nafasi ya kujionea uzuri wa hifadhi hiyo na kujifunza namna wanavyoweza kuchangia maendeleo ya utalii wa mikutano nchini.

"Ziara hii pia, imetuunganisha wataalamu wa rasilimali watu na sekta ya utalii, ikitoa nafasi kwetu kujifunza na kuona fursa za ushirikiano katika utalii wa mikutano.

"Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, ni eneo lenye urithi wa kipekee wa wanyamapori na mandhari za kuvutia, imekuwa kivutio kikubwa kwa wageni wa ndani na wa kimataifa muda wote," alisema.

Juzi, Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana alisema: "Malengo ya wizara yetu kufika mwaka 2025, tunataka tuwe tumeongeza ukusanyaji wa mapato kufikia zaidi ya Dola za Marekani bilioni sita, na watalii zaidi ya milioni tano."

Balozi Chana alisema katika mpango wa kufikia malengo hayo, kwa mwaka 2023 tayari wamekusanya mapato zaidi ya Dola bilioni tatu, hivyo kasi hiyo inahakisi uelekeo wa kufikia malengo yao.

"Tunaamini tutafikia lengo na kuvuka mpaka kufikia mwakani, kwa kuwa mipango iliyoko ni kuhakikisha tunafungua kanda ambazo bado zilikuwa chini kwa masuala ya kiutalii ikiwamo Kanda ya Kusini.

"Tutahakikisha tunaboresha miundombinu ya viwanja vya ndege, barabara na kutangaza vivutio vilivyoko huko, kwa kuwa itachangia kufikia lengo," alisema.

# Ashauri Afrika kuwaendeleza wasimamizi wa rasilimaliwatu

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora-Zanzibar, Haorun Alli Suleiman, amezishauri nchi za Bara la Afrika, kutoa kipaumbele kwa mameneja na wasimamizi rasimaliwatu, kujiendeleza kitaaluma ili kuongeza ufanisi wa kila siku wa watumishi wa umma katika nchi zao.

Sulemain, alitoa ushauri huo jana, wakati akifunga mkutano wa tisa wa mtandao wa mameneja na wasimamizi wa rasilimali watu katika sekta ya umma Afrika (APS-HRMnet).

Mkutano huo unatanguliwa na kauli mbiu, 'Uhimilivu wa utawala na ubunifu kukuza sekta ya umma yenye uelekeo wa baadae kupitia uongozi wa rasilimali watu.'

"Ni wakati muafaka sasa kwa nchi zetu za Afrika kuhakikisha mameneja na wasimamizi rasilimaliwatu kujiendeleza, ili kuongeza ufanisi katika kuwahudumia watumishi wa umma na kuongeza ari katika kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wananchi wetu,"alisema.

Katika hatua nyingine, Suleimani alitoa wito kwa waajiri katika Bara la Afrika kutambua umuhimu wa mkutano huo, kwa kugharamia washiriki kutoka katika chi zao, kwa kuwa una tija kubwa katika kuimarisha sekta ya utumishi wa umma.

"Mafunzo haya ni muhimu sana katika sekta ya utumishi wa umma, hivyo niwaombe waajiri katika nchi zote za Bara la Afrika kutambua umuhimu wa mkutano kwa kutoa ruhusa kwa wajumbe kushiriki mkutano huu, ikiwa ni pamoja na kugharamia gharama zote,"alisema.

Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Zena Ahmed Said, alisema mifumo ambayo imeleta tija katika sekta ya rasilimali watu, kwa baadhi ya nchi ni vizuri nchi nyingine zikajifunza kutoka kwao, ili kuongeza utoaji wa huduma katika sekta hiyo. "Kuna nchi ambazo zimefanya vizuri ikiwamo nchi yetu ya Tanzania katika sekta ya utumishi wa umma ambapo tumepata tuzo ya kimataifa, hivyo ni vema nchi nyingine zikajifunza kutoka nchi zilizofanikiwa," alisema.

Alisema ili kuongeza ufanisi wa sekta hiyo iundwe timu ya wataalam washauri ambao wataandaa mada mbalimbali zitakazowasilishwa katika mkutano wa 10 wa mwaka, kulingana na mahitaji ya wakati huo kwa mameneja na wasimamizi rasilimaliwatu.

Rais wa APS-HRMNet), ambaye pia ni Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-Utumishi wa umma na Utawala Bora, Xavier Daudi, alisema mkutano huo, umekuwa na manufaa makubwa kwa washiriki kubadilishana uzoefu pamoja na kuweka maazimio ambayo yatatekelezwa.

"Maazimio yote tuliyokubaliana niombe kila nchi ikayatekeleze ili mwakani tukikutana nchini Siera Leone utakakofanyika mkutano wa 10 tupate mrejesho wa maazimio yetu,"alisema.

APS-HRMNet, inaundwa na wanachama kutoka Bara la Afrika, ambao wamegawanyika katika kanda tano, ikiwamo Afrika Magharibi yenye nchi 17, Afrika Mashariki nchi 10, Afrika ya Kati nchi nane, Afrika Kaskazini nchi sita na nchi za kusini mwa Afrika 13.

TULIKOTOKA,TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Kukua kwa teknolojia duniani kumesababisha maisha magumu

**Na Adam Fungamwango**



Jiko la Mchina

BINADAMU wamekuwa na maendelea makubwa kutokana na mabadiliko na ukuaji wa teknolojia duniani.

Maisha yamerahisishwa kutokana na kukua kwa teknolojia na dunia imekuwa kama kijiji hivi.

Linalotokea Marekani linaweza kuonekana moja kwa moja nchini kitu ambacho huko nyuma hakikuwepo.

Matokeo ya mechi za Kombe la Dunia, au Mataifa Huru barani Afrika (sasa AFCON), zamani yalikuwa yakitangazwa kwenye redio siku mbili baada ya mchezo kuchezwa, lakini kwa sasa mashabiki wanashuhudia laivu.

Ngoma inachezwa nchini Cameroon, hapa Tanzania watu wako kwenye vinanda umiza wanaitazama kwenye luninga.

Televisheni, simu za mkononi, kompyuta na vitu vingine vinavyofanana na hivyo vimeleta mabadiliko makubwa kwenye maisha ya binadamu na kurahisisha maisha.

Mfano zamani mume akitaka kumsafirisha mkewe kwao au ukweni kusalimia ni lazima ampe pesa ya nauli ya kwenda na kurudia, inawezekana na za matumizi pia.

Ni kwa sababu akishaondoka hakutokuwa na mawasiliano yoyote hadi atakaporudi. Kwa maana hiyo ni lazima awe na nauli ya kurudia ili anapotaka kurudi basi akate tiketi.

Vinginevyo labda mume atume kwa njia ya barua ambayo inaweza kutumia wiki mbili mpaka mwezi hadi kufika.

Vile vile mkiachana mme na mume au wapenzi kwa sababu ya kusafiri hamuwezi kuwasiliana tena wala kujua kama amefika salama au la, mpaka pale mtakapowasiliana kwa barua. Na hiyo pia inategemea kwa wale wenye anuani.

Mambo yamebadilika siku hizi. Mke anapewa nauli ya kwenda tu na posho kidogo ya njiani. Pesa ya matumizi inatumwa baadaye, kesho au siku itakayohitajika. Ni wa sababu wanatumia kutuma kwa njia ya mtandao wa kampuni za simu.

Mwanaume halazimiki tena kumpe mkewe nauli ya kwenda na kurudia. Anaweza kutumia siku moja kabla ya kurejea, inawezekana hata siku hiyo hiyo tu asubuhi akatumiwa na watu wakaenda kukata tiketi. Haya ni maendeleo makubwa nchini ambayo hayakuwepo miaka ya 1995 kurudi nyuma.

Siku zote kila kitu kina faida na hasara yake. Maendeleo ya teknolojia pamoja na faida kubwa na kufanya maisha ya mwanadamu kuwa rahisi, lakini yamesababisha maisha kuwa ghali.

Ni kwa sababu mwanadamu ni lazima alipie gharama za teknolojia hiyo ili makampuni yaweze kujiendesha.

Mfano unapotuma pesa ni lazima kuna makato na tozo, hiyo ni moja kati ya gharama ambazo zinapaswa kukatwa.

Kama zamani ilikuwa ni lazima mtu aende na pesa ya kurudia, lakini kwa sasa makato madogo tu yanawezesha kutuma pesa siku hiyo hiyo hiyo na tiketi ikakatwa kwa nini mtu asitoe. Tena sasa hivi unaweza ukakata tiketi kupitia mtandao na pesa inalipwa kwa mtandao pia.

Zamani hakukuwepo na simu za mkononi, lakini sasa zipo, hivyo kuna gharama za kuinunua, halafu ni lazima uweke vocha na baadaye bando. Wakati zamani kinamama walikuwa wakipigia majiko ya mkaa, mchina na stovu, siku hizi kinamama wengi wanatumia zaidi gesi na majiko ya umeme.

Hapo utaona kuwa kuwa gharama za kujaza gesi, pamoja na kununua umeme kwa ajili ya kupikia.

Zamani hapa nchini hakukuwa na televisheni, siku hizi karibuni nyumba zote za mijini kuna TV, lakini hiyo pekee haitoshi kwani king'amuzi inabidi kilipiwe kwa ajili ya kuangalia mpira, filamu, tamthilia, vikatuni, vichekesho na vingine vingi.

Vitu hivi vyote vinahitaji zaidi uwe na pesa mkononi. Ndiyo maana utaona uhitaji wa pesa kwa sasa ni mkubwa zaidi kwani vitu vingine vinahitaji zaidi fedha kuliko zamani.

Hali hii imesababisha maisha kuwa magumu, kwani yoyote ambaye anataka kumudu hayo ni lazima uwe na pesa, kama baadhi vikikosekana ndipo japo nusu tu, maisha yanaonekana magumu kwani hakuna anayetaka kuishi kama ilivyokuwa zamani, bila simu ya mkononi, televisheni, jiko la gesi na vitu vingi vya kisasa ambavyo ni lazima ugharamie.





Jiko la gesi

**Tuma meseji 0716 350534**

# Trump ateua Mtendaji Mkuu Ikulu

## •Wahamiaji kubanwa, CDC yahofia chanjo

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS mteule wa Marekani, Donald Trump, ameanza kazi ya kuteua baadhi ya viongozi atakaofanya nao kazi, takribani mwezi mmoja kabla ya kuapishwa rasmi.

Amemtangaza meneja wake wa kampeni Susan Summerall Wiles, kuwa Mtendaji Mkuu katika Ikulu ya White House.

Trump alisema katika taarifa yake kwamba, Wiles alimsaidia kufikia ushindi mkubwa zaidi alioupata wa kisiasa katika historia ya nchi hiyo.

Wiles, atahudumu kama mkuu wa utumishi wa Ikulu ya White House, akiwa mwanamke wa kwanza kushikilia wadhifa huo na mteule wa kwanza wa chama cha Republican katika utawala huo mpya unaoingia madarakani.

Kimsingi anatumika kama meneja wa Ikulu ya White House na ana jukumu la kuwaajiri wafanyakazi wa rais.

Pia wanaoshika wadhifa huo, huwaongoza watumishi kupitia Ofisi ya Rais na husimamia shughuli zote za kila siku za wafanyakazi.

Kadhalika wanawashauri marais kuhusu masuala ya sera na wana wajibu wa kuongoza na kusimamia maendeleo ya sera.

Kulingana na kambi ya Trump, Wiles atakuwa mwanamke wa kwanza kuhudumu katika nafasi hiyo.

Susie Wiles, anaelezewa kama mshirika wa kisiasa anayeogopwa zaidi na anayejulikana sana Marekani na vyombo vya habari nchini humo.

Pia, Trump amefanya uteuzi wake wa kwanza wa Baraza la Mawaziri, baada ya ushindi wake katika uchaguzi wa urais, huku akiashiria nia yake ya kuachana na sera ya utawala unaomaliza muda wake.

Wengine wanaotarajiwa kuwa katika mstari wa mbele kujinyakulia nyadhifa katika utawala huo wa Trump ni pamoja na Robert F. Kennedy Jr, kiongozi mkuu katika vuguvugu la kupinga chanjo.

Kwenye suala la chanjo Afrika imetilia shaka iwapo Rais Mteule huyo atatekeleza ahadi ya mtangulizi wake, Rais Joe Biden, ambaye aliahidi kutoa dola milioni 500 na dozi milioni moja za chanjo katika mpango wa kukabiliana na mlipuko wa mpox barani Afrika.

Kituo cha Udhibiti wa Magonjwa Barani Afrika (CDC), kimesema kinatafuta hakikisho toka kwa utawala wa Rais mteule wa Marekani, Donald Trump, ikiwa utatimiza ahadi yake ya ufadhili na chanjo ya mpox iliyoahidiwa na mtangulizi wake.

Aidha wakati huu wagonjwa wa mpox wakiongezeka na maambukizo kuanza kupungua barani Afrika, wafadhili nao wamepunguza kasi ya kutimiza ahadi za kifedha na chanjo, amesema mkurugenzi wa CDC.

Mkurugenzi wa CDC, John Kaseya, alipoulizwa kama ushindi wa Trump unaweza kuathiri uungwaji mkono wa Marekani katika kuchangia huduma za afya barani Afrika, alisema ataufuatilia utawala mpya kutimiza ahadi zilizopo.

Hivi karibuni, Trump alisema atamruhusu mwanaharakati anayepinga masuala ya chanjo Robert F. Kennedy Jr. kufanya maamuzi kuhusu sera ya afya ya Marekani.

Pia Trump ameacha maswali ya kutatanisha, baada ya kuahidi kumpa jukumu kubwa katika sekta ya huduma ya afya na tajiri mkubwa zaidi duniani, Elon Musk, hali inayoakisi sura ya kutatanisha.

Katika mahojiano nadra na Politico, Aprili mwaka huu, alieleza jinsi alivyotoka kutoka asili ya kitamaduni.

"Katika kazi yangu ya mapema mambo kama adabu yalikuwa muhimu na kulikuwa na kiwango kinachotarajiwa cha ustaarabu. Na kwa hivyo ninafahamu kuwa chama cha Republican cha leo ni tofauti.

"Kuna mabadiliko ambayo lazima tuishi nayo, ili tuweze kufanya mambo tunayojaribu kufanya. Lakini watu wanajua kuwa mimi ni mtu thabiti na ninatumai wengi wanajua."

Katika mahojiano yake ya kwanza tangu alipate ushindi wake, Trump alisema hakuna bei kwa mipango yake ya kufukuzwa nchini. Akizungumza na NBC News, alisema:

Kipaumbele chake cha kwanza ni kuimarisha ulinzi wa mpakani na utawala wake ambao hauna budi, kutekeleza kuwarejesha makwao wahamiaji wengi, akidai hilo ndio suluhisho.

Sera yake ya uhamiaji ni baadhi ya masuala yaliyomfanya kupata ushindi huo, Trump alisema na wapigakura walikuwa wanatafuta mgombea atakayewasaidia Wamarekani kwa maarifa.

Trump pia alibainisha jinsi kampeni yake ilivyovutia wapiga kura wengi zaidi katika uchaguzi huo.

Bado hajazungumza na Rais wa Russia, Vladmir Putin, lakini aliongeza kwamba: "Nadhani tutazungumza."

Hata hivyo, Rais Putin amempongeza Trump, kwa ushindi wake wa uchaguzi, akimtaja kuwa mtu jasiri.

Akizungumza katika hafla moja katika mji wa Sochi nchini humo, Putin alisema kuwa Trump alidhulumiwa kutoka pande zote katika muhula wake wa kwanza katika Ikulu ya White House.

Putin pia alisema kuwa madai ya Trump kwamba anaweza kusaidia kumaliza vita nchini Ukraine, yanastahili kuzingatiwa.

Wakati wa kampeni yake, Trump alisema mara kwa mara kwamba, anaweza kumaliza vita hivyo kwa siku lakini hajawahi kufafanua jinsi ambavyo angefanya.

Wakati wa hotuba hiyo, Putin alizungumza kwa saa kadhaa akiangazia mada tofauti. Pia alizungumzia jaribio la kumuua Trump, Julai, mwaka huu, akisema lilimvutia sana.

Wakati wa tukio hilo, baada ya kupigwa risasi, Trump aliinua mkono akiwa amekunja ngumi hewani na kusema maneno pigana, pigana, pigana," kabla ya kuondolewa katika eneo la tukio na maofisa wa huduma ya usalama wa viongozi (Secret Service).

**Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao**



Susan Summerall Wiles, Mtendaji Mkuu Ikulu ya White House, aliyeteuliwa na Rais Mteule wa Marekani, Donald Trump, jana. **PICHA: USA TODAY**

# Othman atoa somo mwenendo mwema

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, ameitaka jamii kuishi kwa kushikamana na kufata mwenendo mwema kwa kuwa ndiko kutekeleza wajibu wa kuilea nafasi ili kufanikiwa katika mambo mbalimbali.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar kupitia kitengo chake cha habari, Othman aliyasema hayo jana huko Shangani Mkokotoni Wilaya ya Kaskazini A Unguja alipowasalimia waumini wa Kiislamu baada ya kuungana nao katika ibada ya swala ya Ijumaa.

Alisema Mwenyezi Mungu amefaradhisha khutuba mbili katika swala ya Ijumaa na ni wajibu wa Waislamu na waumini kuzizingatia na kuzifuata katika kipindi chote cha wiki kwa kuzingatia utekelezaji wa mambo mema kwenye maisha yao.

Makamu aliwaambia waumini hao kwamba kazi ya viongozi ya kusimamia masuala ya nchi ingekuwa rahisi iwapo wanajamii wenyewe wengefuata vilivyo na kuishi katika akhalaki njema kama ilivyoelekezwa katika vitabu na maagizo mbali mbali Dini yao ya uislamu.

Alisema waumini wanapaswa kuishi kwa kuzingatia mambo na taratibu njema ikiwa ndio nyenzo muhimu ya kuiokoa Zanzibar kubakia katika alama zake njema za asili ambazo ni tabia na mweneo mwema kwa watu wake na jamii kwa jumla.

Aidha, Othman alisema ni vyema waumini wakajitahidi kuzinyoosha nafsi zao kama walivyoelekezwa na Quraan na hadithi za kiongozi wa waislamu, Mtume Muhammad (SAW) kwa kuwa kufanya hivyo ndiko kufaulu na kufanikiwa katika maisha ya dunia na ahera.

Makamu wa Kwanza wa Rais alisema kazi ya viongozi waliyopewa na wananchi ya kuilea nchi ingekuwa rahisi iwapo wanajamii wangefuata kikamilifu miongozo na maelekezo ya dini zao na kupata mafanikio.

Naye Katibu wa Swala ya Ijumaa katika msikiti wa Shangani Mkokotoni, Sheikh Said Salum Hamad, aliitaka jamii na waumini kwa ujumla kujiandaa na mauti kwa kufanya mambo mema ambako huko ndio kumcha Mwenyezi Mungu.

Aliwakumbusha Waislamu kuacha matendo mabaya na kufuata mwendo mwema pia kuyachukulia mauti kuwa ni mawaidha kama ilivyoelekezwa na Mtume Muhammad (SAW).



Mkurugenzi wa Wateja Binafsi wa Benki ya Stanbic Tanzania, Omari Mtiga akizungumza wakati akitoa maoni yanayohusu familia, mitindo ya maisha na mahitaji binafsi ya kibenki, wakati wa hafla iliyojulikana kama 'Private Banking CVP', jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## CCM kuwawekea pingamizi wote wasiokidhi vigezo

**Mussa Mwangoka, MPANDA**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Katavi, kimesema kitawawekea pingamizi wagombea wa vyama vingine vya siasa ambao hawajakidhi vigezo vya kushiriki uchaguzi.

Akizungumza na waandishi wa habari, Katibu Siasa na Uenezi wa CCM Mkoa wa Katavi, Teonas Kinyoto, alisema wamejipanga kushinda kwa kishindo katika uchaguzi huo.

Alisema wamesimamisha wagombea katika maeneo yote kuanzia nafasi za wenyeviti na wajumbe wa mitaa, vitongoji na avijiji.

Alisema hawatosita kuwawekea pingamizi wagombea wa wasio na sifa stahiki waliosimamishwa na vyama vingine ambao watabainika kukiuka kanuni na taratibu za uchaguzi huo.

"Tuna taarifa wenzetu wamesimamisha wagombea ambao hawana sifa stahiki kwa mujibu wa taratibu za uchaguzi, hatutaacha kuwawekea pingamizi" alisema.

Kinyoto alitumia nafasi hiyo kukanusha taarifa za kwamba, CCM imetumia viongozi wake wakiwamo wakuu wa wilaya kuwatisha wagombea wa upinzani kiasi kwamba, baadhi yao walijitoa katika kinyang'anyiro cha kugombea nafasi za uongozi.

Kauli hiyo, imekuja kukiwa kuna malalamiko kutoka viongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) na ACT-Wazalendo ngazi ya mkoa wakidai kukosa wagombea kutokana na wale waliotegemea kugombea kutishwa na Viongozi wa CCM na Serikali.

Viongozi ambao ni Mwenyekiti wa ACT Wazalendo, Joseph Mona na Rhoda Kunchela wa CHADEMA kwa nyakati tofauti walilalamikia CCM kufanya mchezo mchafu dhidi ya vyama vyao.

# Pinda asema mamlaka mtandao ni muhimu kwa usalama wa nchi

**Na Lusungu Helela**

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deus Sangu, amesema Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ni taasisi nyeti kwa ajili ya usalama wa nchi.

Amesema hakuna mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) uliosanifiwa unaoweza kutumika nchini katika wizara, taasisi au idara ya serikali bila kuridhiwa na e-GA

Pinda alisema hayo juzi jijini Dodoma wakati akizungumza na wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria katika kikao cha kamati hiyo na watendaji wa e-GA na taasisi ya uongozi

Kikao hicho kililenga kupokea na kujadili taarifa ya utendaji kazi wa taasisi hizo huku akibainisha kwamba tangu kuanzishwa kwake, e-GA imeleta mageuzi makubwa huku akitaja mifumo mingi inayotumika kwa sasa serikalini imebuniwa na kusanifiwa na mamlaka hiyo,

Alisema ujio wa e-GA umeisaidia kupunguza gharama kubwa kwa serikali kulinganisha na awali ambapo mifumo mingi iliyokuwa ikitumika kwenye taasisi za serikali ilikuwa ni ya kutoka nje, akitolea mfano mfumo wa ununuzi wa TANEPS ulikuwa ukimlazimisha mtumiaji kama anataka kufanya marekebisho ni lazima awasiliane na watengenezaji wa mfumo ambao ni Wagiriki

" Kama nchi kulikuwa hakuna usiri wa taarifa zetu. Wasanifishaji mifumo ya TEHAMA ambao ni wa kutoka mataifa ya nje ndio walikuwa wenye 'server' za taarifa zetu," alisema Sangu

Alisema awali taasisi nyingi za serikali zilikuwa zikitumia mifumo hiyo ya kutoka nje bila kuidhinishwa na e-GA na ilikuwa rahisi kuhujumu kwa lengo la kujinufaisha kwa kushirikiana na watu wa kutoka nje ila kwa sasa hilo jambo haliwezekani kutokana na uwepo wa e-GA

"Upo ushahidi kabisa kwamba e-GA imesaidia kuboresha utendaji kazi, imeimarisha utawala bora, kupunguza vitendo vya rushwa ambavyo vingeweza kujitokeza, kuimarisha makusanyo na kudhibiti matumizi ya maduhuli ya serikali," alisisitiza.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Utawala, Katiba na Sheria, Dk. Joseph Mhagama, aliipongeza e-GA kwa kazi kubwa inayoendelea kuifanya huku akiitaka kjiimarisha zaidi kwenye eneo la ubunifu ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia yanayotokea dunia kote

Dk. Mhagama aliitaka e-GA kusanifu mifumo itakayosaidia kupunguza matatizo katika jamii ikiwemo upotevu mkubwa wa maji unaotokea katika maeneo mbalimbali nchini.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.
Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.
Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile.
Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani.
Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-38

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Wakati narudi ile kukata kona, nikamuona yule jamaa ametoa kitu kama chuma hivi akampiga nacho dada mmoja kichogoni. Alikuwa anatoka nyumbani wake, alikuwa amemalizika kufunga kigeti cha nje ya mlango wake. Yule mdada akaanguka chini. Haraka akatokea mtu mwingine aliyetokea upande mwingine, wakambeba haraka sana. Mimi nilijibanza sehemu ili wasinione. Nikanyata na kuwafuatilia. Nikawaona wanamuingiza kwenye gari. Kusema ukweli sikuweza kufahamu kama walimuua pale pale, au alikufa baadaye.

Sikumwambia mtu lile tukio kwa sababu lilikuwa ni la kutisha na kuogofya, pia niliogopa kuisaidia polisi maana ingeonekana mimi nimeliona lakini hakuna mtuhumiwa aliyekamatwa.

Kesho yake tukasikia yule mdada ambaye mimi namfahamu amefariki kwa kuanguka kwenye mtaro mmoja wakati anafanya mazoezi kwa mshtuko wa moyo, nilishangaa sana, lakini ilikuwa ni siri yangu.

Baada ya wananchi na ndugu kukataa ripoti nilidhani kuwa italetwa ya tukio ambalo linalifahamu, lakini ikasemwa kuwa mchumba wake Kamal ndiyo kamuua.

Haikuwa kweli, mimi mchumba wake namfahamu sana, huwa anafika mara kwa mara pale. Na aliyempiga na chuma namfahamu ni huyo hapo mheshimiwa jaji, aliyekuja kumsaidia kubeba huyo hapo mwingine, wote niliwakariri kabisa. Waliobaki kusema kweli mimi siwajui." Ulikuwa ushahidi wa Bakari.

Baada ya kupokea ushahidi huo, mahakama iliutaka ushahidi wa daktari Dancun Shija.

Mbali na kuwa ni mmoja wa madaktari waliofanya uchunguzi wa ripoti ya pili ambayo jumba bovu lilimuangukia Kamal kuonekana muuaji, lakini ndiye aliyekuwa mtu wa kwanza kuonana na Kamal alikuwa amejificha kwenye hospitali yake binafsi pale Ilala ili asikamatwe.

Alijifanya mgonjwa ili alale pale kwa siku kadhaa, lakini lengo lilikuwa ni kukimbia kukamatwa na kupumzisha kichwa kutokana na kuamini kuwa sehemu pekee ambayo askari huwa hawatafuti wahalifu au watuhumiwa ni hospitali. Labda mtu huyo awe mpelelezi mzoefu na mbobezi, tena aliyepata taarifa za kiitelejensia. Ushahidi wa dokta Shija uliendelea na mahakama ikapata habari yote jinsi Kamal alivyofika hospitalini hapo maeneo ya Ilala akijifanya




**"Kwani unajisikiaje, huna nguvu?" "Siyo kama sina nguvu na kizunguzungu juu." Kamal alimjibu nesi aliyempokea. Hakukuwa na daktari kwa muda huo. Alipokuja alimpima lakini hakumkuta na ugonjwa wowote.**

anaumwa.

Alimkuta mhudumu, akamwambia anajisikia vibaya, hivyo anaomba kitanda alazwe.

"Kwani unajisikiaje, huna nguvu?" "Siyo kama sina nguvu na kizunguzungu juu." Kamal alimjibu nesi aliyempokea. Hakukuwa na daktari kwa muda huo. Alipokuja alimpima lakini hakumkuta na ugonjwa wowote.

"Nadhani ni uchovu na kufanya kazi bila kumpumzika, lakini tumekupima kila kitu, unaonekana hauna tatizo." "Sawa lakini nasi bado najisikia vibaya, tena kichwa ndiyo kabisa." "Basi endelea kumpumzika." Alipoondoka alipoondoka, alimwita nesi na kumwambia lengo lake ni kupumzika pale kwa siku tatu. "Nataka nipumzike kwa sababu nina msongo wa mawazo, sitaki kurudi uraiani, nina matatizo kwenye familia yangu. Pia naomba unifunge bandeji kichwani kama mtu aliyeumia ili sura yangu usionekana vyema. Ndugu zangu wanaweza kunitafuta mahospitalini na zahanati wakanikuta hapa."

Shija akaiambia mahakama kuwa kwa siku kadhaa alizokaa pale tayari walikuwa wamemzoea, lakini hakujua kama ni mtu anayetafutwa na polisi kwa mauaji kwa sababu alijibadilisha sura alikuwa na nywele nyingi na kupenda kuvaa miwani ya jua, tofauti na sura iliyokuwa kwenye gazeti iliyotolewa na polisi kuwa anatafutwa ambayo alikuwa amenyoa upara.

"Mheshimiwa Jaji, tulimuona ni mmoja wa watu ambao wameikimbia tu familia yake, amemua kukaa sehemu ambayo haitaji bugudha kutokana na msongo wa mawazo na si yule mtuhumiwa na mauaji ya mchumba wake.

Dokta Shija aliiambia mahakama siku aliyokuja kugundua hilo ni baada ya Kamal kujitambulisha mwenyewe na pale alipojua kuwa yeye ni mmoja wa madaktari waliomfanyia uchunguzi marehemu Mariamu kwenye Hospitali ya Rufaa.

"Alisikia siku moja nikiongea na mtu aliyekuja ofisini kwangu, juu ya ripoti ya kifo cha mwanamke mmoja aliyesemekana ameuawa. Alijua kabisa anayezungumzwa ni Mariamu.

********************************

"Naitwa Kamal, mimi ndiye mchumba wa Mariamu, aliyeanguka kwa presha au kuuawa. Baadaye ikasemekana ameuawa na mpenzi wake.

"Nadhani sasa dokta utaelewa au kufahamu kwa nini mimi nilikuja hapa kuomba 'hifadhi.' Ni kwa sababu ya kuhofia kukamatwa. Dunia nzima inajua kuwa mimi ni muuaji. Lakini ukweli uliopo moyoni mwangu ni kwamba mimi sijamuua mpenzi wangu. Nina simanzi ya kuuawa kwa mchumba wangu, walimwengu wakaniongezea uchungu mwingine wa kunisingizia uuaji."

"Kumbe wewe ndiye mchumba wa yule binti!?" Nilimuuliza. "Hilo ni jibu dokta."

"Mimi niliamuni haraka kwa sababu uchunguzi wa madaktari wa kwanza wa madaktari wenzetu ulipingwa na ndugu na wananchi, hata sisi tulivyofuatilia tuligundua kulikuwa na shinikizo lilitokana na rushwa, lakini ukweli ilikuwa ni ripoti ya uongo.

Sisi wenyewe madaktari baada ya uchunguzi wa pili tukaanza kuulizana, ilikuwaje ikawa hivyo? Ndiyo tukapata taarifa za uhakika kuwa waliomuua ndiyo waliotumia pesa ili kupindisha uchunguzi wa kwanza. Na hao hao walitaka kushinikiza uchunguzi wa pili uwe kama wa kwanza, tukakataa. Tukautoa kama ilivyo. Tukapata taarifa sasa kuwa wale wale jamaa, wamekwenda kutoa pesa kwa baadhi ya askari polisi wasio waaminifu wamsingizie mtu mwingine kesi ya mauaji baada ya taarifa sahihi kutoka na kuwaridhisha ndugu na wananchi. Nilishangaa na kupatwa na simanzi niliposikia eti 'aliyepewa kesi ya kichwa', ni mchumba wake. Kwa maana hiyo binafsi niliingiwa na huruma sana. Ndiyo maana alipojitambulisha nikamuahidi kuwa nitamsaidia kwa hali na mali hadi ukweli ujulikane," Dokta Shija bado aliendelea kutoa ushahidi mahakamani.

Akasema kutokana na hilo alikwenda kumshirikisha mdogo wake ambaye ni askari polisi aliyekuwa ndiyo kwanza anaanza kazi kama miezi sita tu iliyopita kuhusu jambo hilo.

"Kwa sababu nilimwambia mtu huyu mimi nataka kumsaidia na yeye akasema atatumia taaluma yake ya upolisi ili kumsaidia ingawa kwa kificho kwa sababu hatari Jeshi la Polisi limeshamuweka kuwa mtuhumiwa, hivyo alifanya kazi kwa kificho ili kusaka ukweli bila kuwashirikisha waajiri wake, hadi walipombaini bosi wa Kamal ndiyo anahusika, jinsi walivyofanya nadhani shadihi wa nne, mdogo wangu Willy Shija atakuja kuelezea zaidi."

*Itaendelea Jumamosi*

## Wachezaji Fountain Gate FC kikaangoni

**Na Adam Fungamwangwo**

BAADA ya kupata kipigo cha mabao 3-1 kutoka kwa Pamba Jiji, wachezaji wa Fountain Gate waliitwa katika kikao maalumu ili kujadili matokeo hayo pamoja na hatima ya timu hiyo kuelekea michezo inayofuata ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ofisa Habari wa Fountain Gate, Issa Mbuzi, alisema uongozi ulikutana na wachezaji baada ya mechi hiyo iliyochezwa Jumanne iliyopita kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Manyara ili kufahamu sababu ya kupokea kipigo hicho cha kwanza wakicheza nyumbani.

"Sisi kama viongozi tumeshakutana na wachezaji kuulizana, kukubaliana na kutiana moyo kwa sababu kwenye soka siyo kila siku utakuwa na furaha, kuna wakati ni lazima utakuwa na huzuni.

Vikao vimefanyika vya ndani ili kuhakikisha tukirejea kutoka kwenye mapumziko ya Kalenda ya Kimataifa ya FIFA, turudi kwa ari mpya, ili mechi zote ambazo tutacheza kwenye uwanja wa Tanzania Kwaraa, tusiwape karaha mashabiki wetu kama ambavyo imetokea kwenye mchezo wetu dhidi ya Pamba, unajua hawajazoea, yamewaumiza sana," alisema Mbuzi.

Ofisa huyo alisema kwa sasa kikosi kimeanza mazoezi kujiandaa na mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga ambao utachezwa Novemba 21, mwaka huu jijini,Dar es Salaam.

"Mechi inayofuata tunakuja kucheza na Yanga, tunajua haitakuwa mechi rahisi, tunatakiwa kujipanga na kujiimarisha katika kila idara ili kupata matokeo mazuri, hakuna mechi nyepesi," Mbuzi aliongeza.

Fountain Gate iliyocheza michezo 11, ikishinda mitano, sare mbili, ilikuwa imepoteza michezo mitatu lakini nje ya uwanja wake wa nyumbani, kwa mara ya kwanza imefungwa kwenye uwanja huo kwa timu ambayo haikutarajiwa.

Ilikuwa imecheza michezo mitano kwenye uwanja huo, ikishinda mitatu na sare mbili kabla ya kipigo hicho.

Katika msimamo wa ligi timu hiyo, Fountain Gate ipo katika nafasi ya tano, ikikusanya pointi 17, ikifunga mabao 20 na kuruhusu 20, ikiwa moja ya timu zilizofunga mabao mengi kwenye ligi, lakini yenyewe vilevile nyavu zake zikitikiswa mara nyingi.

# MWEMBE MAKUMBI CITY KILELENI LIGI KUU ZANZIBAR

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MWEMBE Makumbi City imeendelea kujiimarisha baada ya kuifunga Junguni United mabao 3-1 katika mechi ya raundi ya 10 ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa juzi visiwani hapa.

Mchezo huo uliokuwa na ushindani ilifanyika kwenye Uwanja wa Mau A na kuhudhuriwa idadi kubwa ya mashabiki ambao walikuwa wakiishangilia Mwembe Makumbi City.

Kwa matokeo hayo Mwembe Makumbi City imetinga kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar baada ya kufikisha alama 22 huku nafasi ya pili ikichukuliwa na Mlandege FC yenye pointi 20 sawa na Mafunzo FC wanaofuatia katika msimamo huo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Junguni United, Damian Mussa, alisema timu yake ilicheza vizuri lakini makosa madogo katika safu ya ulinzi ndio iwafanya kuadhibiwa na wapinzani wao.

Damian alisema safu yake ya ulinzi ilishindwa kufanya mawasiliano sahihi na kusababisha kuruhusu mashambulizi kueleekezwa katika lango lao.

Kocha huyo alisema kitu kikubwa walichowazidi wapinzani wao ni mfumo wa mashambulizi hasa pale wanapomiliki mpira jambo lilipelekea timu yake kushindwa kuumudu mchezo huo.

"Kiujumla timu imecheza vizuri sana, sina lawama na wachezaji wangu ila tu hatukuwa bora katika eneo la ulinzi, makosa madogo ya kupoteza umakini na kushindwa kudhibiti mbinu za wapinzani wetu ndio yamepelekea tufungwe," alisema kocha huyo.

Aliongeza dakika zote za mchezo wachezaji wake walijaribu mara kadhaa kupeleka mashambulizi katika lango la wapinzani wao lakini walishindwa kupata bao na kupelekea kupokea kipigo hicho.

"Tunarejea nyumbani Kisiwani Pemba kujipanga na mchezo iliyobakia ili kuhakikisha tunapata ushindi kati ya michezo mitano ya kukamilisha mzunguko huu wa kwanza," aliongeza Damian.

Katika mechi nyingine ya ligi hiyo, JKU SC ilizinduka na kupata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Chipukizi, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau B juzi jioni huku kwenye Finya, Maafande wa Uhamiaji walijikuya wakigawana pointi na Tekeleza kwa kumaliza dakika 90 wakiwa na sare ya bila kufungana.

Wakati huo huo, Shekha Khamisi wa Mafunzo SC, Hassan Pele kutoka Mlandege na Damian Mussa anayeingoza Junguni United wanawania Tuzo ya Kocha Bora wa Oktoba.

Wachezaji wanaowania Tuzo ya Mchezaji Bora wa Oktoba ni pamoja na Matheo Andrea kutoka Mafunzo, Abdallah Iddi 'Pina' anayeichezea Mlandege na Shomary Kibwana wa Junguni United.



Mshambuliaji wa Simba Queens, Precious Christopher, akifanya mazoezi huku Kocha Mkuu wa timu hiyo, Yussif Basigi, akifuatilia kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania dhidi ya Yanga itakayochezwa Novemba 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam. **PICHA: SIMBA SC**

# Mashujaa kuimarisha ukuta wao

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kuhakikisha hawaruhusu nyavu zao kutikiswa kirahisi, benchi la ufundi la Mashujaa FC limesema litaimarisha mabeki wake kwa kuandaa programu maalumu itakayowajenga na kuwarejeshea ubora wao, imeelezwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Mashujaa, Abdallah Mohamed 'Bares' alisema kikosi chake kimeshindwa kupata matokeo bora katika baadhi ya mechi zilizopita kutokana na safu yao ya ulinzi kuruhusu magoli mepesi.

Bares alisema atawajenga upya mabeki wake na kuwataka kuongeza umakini wakati wote mpaka pale watakaposikia filimbi ya mwisho ya mwamuzi.

"Kipindi hiki cha mapumziko nitakuwa na kazi ya kuboresha safu yangu ya ulinzi ambayo nimebaini katika mechi iliyopita imeonyesha mapungufu, naamini tutarejea vizuri na kila kitu kitakaa sawa," alisema Bares.

Kocha huyo alisema Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu ina ushindani mkubwa tofauti na msimu uliopita na wanaahidi kuendelea kupambana ili wamalize katika nafasi za juu katika msimamo wa ligi hiyo yenye timu 16.

"Malengo yangu ni kushika nafasi ya juu katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, tunatarajia kufanya vyema katika michezo yetu yote iliyobakia," Bares aliongeza.

Wakati huo huo, Bares amempongeza Kaimu Kocha Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Hemed Suleiman 'Morocco' kwa uteuzi wa kikosi imara kuelekea michezo ya kusaka tiketi ya kucheza Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2025).

## ZISIKUPITE

### MBEUMO ATAJWA NEWCASTLE

NEWCASTLE United imeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa Brentford na Timu ya Taifa ya Cameroon, Bryan Mbeumo,mwenye umri wa miaka 25, Januari lakini Magpies wanakabiliwa na vikwazo vya matumizi ya fedha. ***(Telegraph)***

### CITY YAMWAZA GUARDIOLA

KLABU ya Manchester City imesema inamatumaini, Pep Guardiola, ataongeza muda wake kama kocha na klabu hiyo ya Ligi Kuu England. ***(Mail,}***

### UNITED PESA KIDUCHU

YOYOTE atakayemrithi Erik ten Hag kama Kocha wa Manchester United atakuwa na bajeti ndogo ya kuimarisha kikosi katika usajili wa dirisha dogo litakalofunguliwa ifikapo Januari. ***(Guardian)***

### DAVIES AICHAGUA MADRID

KLABU ya Manchester United imeonyesha nia ya kumsajili beki wa pembeni wa Bayern Munich mwenye umri wa miaka 23, Alphonso Davies, lakini mchezaji huyo yuko mbioni kuhamia Real Madrid**. *(Sky Sports Switzerland, Via Give Me Sport)***

### ROGERS MAMBO MAZURI

KLABU ya Aston Villa inakaribia kuafikiana na mshambulizi, Morgan Rogers,mwenye umri wa miaka 22 kuhusu mkataba mpya. ***(Football Insider)***

### SANE AKARIBIA ARSENAL

KLABU ya Arsenal inashughulikia mpango wa kumsajili winga wa Ujerumani, Leroy Sane mwenye umri wa miaka 28, wakati mkataba wake wa Bayern Munich utakapokamilika msimu ujao**. *(Football Insider)***,

### CITY, LIVERPOOL VITANI

KLABU ya Sporting iko tayari kumuuza Viktor Gyokeres kwa dau la kuanzia pauni milioni 50 hadi 58 ifikapo msimu ujao, huku Manchester City, Arsenal, Liverpool na Chelsea zikimhitaji mshambuliaji huyo wa Sweden mwenye umri wa miaka 26. ***(Florian Plettenberg),***

### ANTONY SOKONI EPL

KLABU ya Manchester United itapunguza hasara yao kwa winga wa Brazil Antony mwenye umri wa miaka 24, kwa pauni milioni 86 baada ya Erik ten Hag kutimuliwa. ***(Sportsport)***

### SPURS KUMTOA WERNER

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Ange Postecoglou, anategemea kumtoa fowadi Mjerumani, Timo Werner,mwenye umri wa miaka 28, mwishoni mwa msimu. ***(GiveMeSport)***

### WEST HAM HAKIJAELEWEKA

KLABU ya West Ham haina uwezekano wa kuwa na fedha za kutumia katika dirisha la usajili la Januari. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MBAPPE ATEMWA UFARANSA

## Ni kuelekea mechi za UEFA dhidi ya Italia na Israel huku...

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe hajajumuishwa katika kikosi cha Ufaransa kwa ajili ya mechi za Ligi ya Mataifa ya Uefa dhidi ya Israel na Italia, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Didier Deschamps, alithibitisha.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 25 amekosolewa kwa uchezaji wake tangu ajiunge na Real Madrid msimu wa joto, huku klabu hiyo ya Hispania ikiwa nyuma ya Barcelona kwa pointi tisa kwenye LaLiga na kusalia katika nafasi ya 18 kwenye jedwali la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Neymar alikosa mechi mbili za Ufaransa mwezi uliopita, dhidi ya Israel na Ubelgiji.

"Nimekuwa na mazungumzo naye, ni uamuzi ambao nilichukua kwa safu hii ya mechi pekee," alisema Deschamps akiuambia mkutano na waandishi wa habari.

Licha ya ukosoaji huo, Mbappé amefunga mabao sita na kutoa asisti moja katika mechi 10 kwa klabu yake mpya, lakini amekuwa na wakati mgumu kutengeneza uhusiano wenye tija na nyota mwenzake wa Madrid, Vinícius Júnior.

"Huenda tusikubaliane kwa kila kitu," alisema Deschamps.

"Haya ni majadiliano naweza kufanya na wachezaji, siko hapa kuambiwa na wachezaji kuwa mimi ni bora na mzuri zaidi. Ninawasikiliza. Nimekuwa nikihamasishwa na mijadala hii, iwe ya kibinafsi au kwa pamoja, kuwalinda wachezaji wote.

"Ndio maana naweza kuwa na mijadala mingi ambayo inaweza kwenda zaidi ya uwanja, kwa sababu wanajua vizuri kuwa tunajua ni nani aliyezungumza ikiwa kitu kitatokea. Mabadilishano haya ni muhimu kwangu. Kwa faida ya kutazama nyuma, utulivu na kama uwazi zaidi iwezekanavyo, nafanya maamuzi ambayo yanaonekana bora kwangu."

**Kikosi kamili cha Ufaransa:**

**Makipa:** Mike Maignan (AC Milan), Brice Samba (Lens) na Lucas Chevalier (Lille)

**Mabeki:** Jonathan Clauss (Nice), Lucas Digne (Aston Villa), Wesley Fofana (Chelsea), Theo Hernández (AC Milan), Ibrahima Konaté (Liverpool), Jules Koundé (Barcelona), William Saliba (Arsenal), Dayot Upamecano (Bayern Munich).

**Viungo:** Eduardo Camavinga (Real Madrid), Matteo Guendouzi (Lazio), N'Golo Kanté (Al Ittihad), Manu Koné (Roma), Adrien Rabiot (Marseille), Warren Zaïre-Emery (Paris Saint-Germain)

**Washambuliaji:** Bradley Barcola (PSG), Ousmane Dembélé (PSG), Randal Kolo Muani (PSG), Christopher Nkunku (Chelsea), Michael Olise (Bayern Munich), Marcus Thuram (Inter Milan)

## HABARI MICHEZO

# Hatimaye Ortega aitwa Ujerumani

**BERLIN, Ujerumani**

MLINDA mlango namba mbili wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu England Manchester City, Stefan Ortega,ameitwa kwa mara ya kwanza katika kikosi cha Timu ya Taifa ya Ujerumani kinachoingia kambini kujiandaa na mechi za Ligi ya Mataifa ya Ulaya.

Ortega mwenye umri wa miaka 32 ameitwa katika kikosi cha timu hiyo sambamba na mlinda lango wa Stuttgart, Alexander Nuebel na Oliver Baumann kutoka katika Klabu ya Hoffenheim.

Hii ni kutokana na golikipa namba moja wa kikosi hicho na FC Barcelona, Marc-Andre Ter Stegen kukosekana kutokana na jeraha la goti.

Ujerumani itakuwa mwenyeji wa wa Bosnia and Herzegovina Novemba 16, mwaka huu mjini Freiburg ahalafu itasafiri hadi Budapest kukipiga dhidi ya Hungary siku tatu baadaye.

Hata hivyo, taifa hilo lilishafuzu robo fainali ya michuano hiyo, baada ya sare moja na ushindi wa mechi tatu.

Pamoja na Ter Stegen,Ujerumani wataendelea pia kuwakosa fowadi wa West Ham Niclas Fullkrug, Jamie Leweling wa Stuttgart, kiungo wa Bayern, Aleksander Pavlovic, Leroy Sane na kiungo,David Raum wa RB Leipzig.




# Pau aishusha presha Barcelona

**BARCELONA, Hispania**

TAARIFA kutoka Barcelona zinaeleza beki wa klabu hiyo, Pau Cubarsi,anaendelea vizuri baada ya kupata jeraha usoni lililotokana na kugongwa na mguu wa beki wa kati, Uros Spajic wa Red Star Belgrade ya Serbia katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Cubarsi mwenye umri wa miaka 17 alionekana kuvuja damu baada ya tukio hilo kabla ya kutolewa dakika ya 67.

Katika mchezo huo wa Jumatano usiku Barcelona ikishinda mabao 5-2, Robert Lewandowski, akitupia mawili na mebngine yakipachikwa na Inigo Martinez, Raphinha na Fermin Lopez.

Kocha wa kikosi hicho, Hansi Flick, amesema kinda huyo alihitaji kushonwa nyuzi 10 na anaendelea vizuri kabla ya ukurasa rasmi wa klabu hiyo kuposti picha yake akitabasamu ikiwa na maneno 'niko sawa'.

Cubarsi ambaye ni zao la shule ya vipaji ya Barcelona ya La masia alianza kukitumikia kikosi cha kwanza cha akiwa na miaka 16 katika mchezo wa Copa del Rey dhidi ya Unionistas de Salamanca Januaro 18, mwaka huu.

Tangu kipindi hicho amekuwa sehemu muhimu katika kikosi hicho na kujiamini katika eneo lake.







# KUDUS APATA ADHABU ZAIDI

**LONDON, England**

CHAMA cha Soka England (FA) kimemwongezea adhabu winga wa West Ham United, Mohammed Kudus, inayotokana na kadi nyekundu aliyoonyesha katika mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Tottenham Hotspur iliyopigwa Oktoba 19, mwaka huu.

Kudus sasa atakosa mechi tano badala ya tatu.

Katika mchezo huo Kudus alimchezea faulo beki wa kati wa Spurs, Micky van de Ven dakika ya 83 jambo lililozua tafrani, beki huyo mholanzi akidai Kudus alimtwanga ngumi usoni.

Kudus alipewa kadi ya njano kwa tukio hilo kabla ya mwamuzi,Andy Madley, kubadilisha uamuzi wake na kumpa kadi nyekundu baada ya tukio hilo kupitiwa upya na waamuzi wa VAR.

Winga huyo tayari amekosa mechi dhidi ya Manchester United na Nottingham Forest na alikua akimaliza adhabu hiyo wikiendi hii dhidi ya Everton.

Lakini sasa ongezeko la adhabu hii litamfanya kukosa mechi dhidi ya Newcastle United itakayochezwa Novemba 25 na dhidi ya Arsenal siku tano baadaye.

# CAMARA AMFUNIKA DIARRA KWA CLEAN SHEETS LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA wa Simba, Moussa Camara, anaongoza kwa kukaa langoni mechi nyingi bila kuruhusu bao katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara hadi kufikia raundi ya 10.

Mpaka sasa ambapo mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara zimesimama kupisha Kalenda ya Kimataifa, Camara, ambaye pia ni kipa wa Timu ya Taifa ya Guinea, hajaruhusu wavu wake kutikiswa mara nane katika michezo 10 ambayo amekaa langoni.

Kipa huyo aliyesajiliwa msimu huu akitokea kwenye Klabu ya Horoya ya Guinea, amekaa langoni katika michezo yote ambayo Simba imecheza kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Kwa mujibu wa dawati la takwimu za michezo za gazeti hili, alizipata aliposimama langoni Simba na kutoruhusu wavu wake kuguswa kwenye michezo dhidi ya Tabora United, timu yake ikishinda mabao 3-0, Fountain Gate mabao 4-0, Azam FC 2-0, Dodoma Jiji bao 1-0, Prisons bao 1-0, Namungo mabao 3-0, Mashujaa FC bao 1-0 na KMC mabao 4-0.

Ni mechi mbili tu ambazo amekosa ‚clean sheets' kwa kuruhusu mabao mawili, Simba ilipotoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Coastal Union na kupigo cha bao 1-0 dhidi ya Yanga.

Camara anafuatiwa na kipa wa Yanga, Djigui Diarra, ambaye ni kipa wa Timu ya Taifa ya Mali, anayeshika nafasi ya pili akiwa na ‚clean sheets' saba katika michezo tisa aliyocheza.

Alizipata kwa timu yao kushinda mabao 2-0 dhidi ya Kagera Sugar, KenGold bao 1-0, KMC bao 1-0, Pamba Jiji mabao 4-0, Simba bao 1-0, JKT Tanzania mabao 2-0 na Singida Black Stars bao 1-0.

Kipigo ilichokipata juzi Yanga cha mabao 3-1 dhidi ya Tabora United, kimemfanya kukaa langoni mechi mbili bila ‚clean sheets', kwani pia Jumamosi iliyopita aliruhusu bao 1-0 dhidi ya Yanga.

Wakati Yanga ikicheza michezo 10 katika ligi hiyo, Diarra hakukaa langoni kwenye mchezo mmoja ambao timu yake ilicheza dhidi ya Coastal Union, badala yake Khomeiny Aboubakar, alisimama langoni, hivyo kumfanya Diarra kukaa langoni michezo tisa tu.

Kipa wa Singida Black Stars, Metacha Mnata anashika nafasi ya tatu akiwa na ‚clean sheets' sita akikaa langoni kwenye michezo yote 10 ambayo timu yake imecheza.




Kikosi cha USA Stars kikiwa kimebeba kombe baada ya kutwaa ubingwa wa mashindano ya Ligi ya Vijana ya umri chini ya miaka 15 ya mkoa wa Arusha. USA Stars iliwafunga Upendo Friends FC bao 1-0 katika mechi ya fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ngarasero Arumeru mapema wiki hii. **PICHA: ARFA**

# Wasanii wa tamthilia kuchuana

**Na Mwandishi Wetu**

KWA mara ya kwanza nchini, wasanii wa tamthilia wanatarajia kuchuana kuwania tuzo zitakazofanyika Desemba, mwaka huu.

Mkurugenzi wa tuzo hizo, Eliya Mjata, alisema lengo la kuanzisha tuzo ni kutambua na kuenzi mchango pamoja na jitihada zinazofanya na wasanii huku akieleza mchakato wa kupiga kura utaanza Novemba 18, mwaka huu.

Mjata alisema tuzo hizo zitatoa fursa ya kujitangaza kwa waigizaji, watayarishaji, waandishi wa muziki, wabunifu wa mavazi na mapambo.

"Mchakato wa upigaji kura utajumuisha wadau mbalimbali ikiwamo watazamaji wa tamthilia wanaohusika na uzalishaji wa kazi hizo na wataalamu kutoka sekta ya filamu," alisema Mjata.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Filamu wa Bodi ya Filamu Tanzania, Emmanuel Ndumukwa, alisema kupitia tuzo wanatarajia kuona ushindani na ubora wa kazi unaonekana.

"Hiki ndicho cha kwetu tukipende, Watanzania endeleeni kuwasaidia wasanii kwa kununua kazi zao na kutazama zaidi filamu za ndani," alisema Ndumukwa.

## Gamondi abeba lawama Yanga

INATOKA UK. 24

Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

"Hakuna mchezo mwepesi, tumeumia kufungwa lakini lazima tukubali upinzani uliopo, kwa sasa ligi itasimama kupisha majukumu ya timu za taifa, tutarejea kwa nguvu.

Kila kitu leo (juzi), kilikwenda vibaya, tumepata majeruhi dakika ya nane tu, Kennedy Musonda amepoteza nafasi ya wazi, tumepoteza penalti na wao wamefunga, wameshambulia mara mbili tu wakafunga mara zote, sisi tumeshambulia zaidi ya mara tatu hatukufunga, mara nyingi timu ikishinda kila mtu anakuwa na furaha, lakini ikifungwa lawama zinabaki kwetu, siwezi kupeleka lawama kwa wachezaji wangu, zote nazibeba mimi," aliongeza kocha huyo.

Alisema pia anapata wakati mgumu wa kutekeleza programu za kufanyia kazi mapungufu kwa sababu idadi kubwa ya wachezaji wake wanakwenda katika majukumu ya kimataifa.

"Wachezaji hawapumziki, bado kuna kalenda ya kimataifa, wachezaji watasafiri nchi mbili hadi tatu, huwa ninabakia na wachezaji wasiozidi wanne wa kikosi cha kwanza, na wakirudi ni kama tunaanza upya," alilalamika Gamondi.

Kipigo hicho cha juzi kimeifanya Yanga yenye pointi 24 kukaa katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara huku watani zao, Simba wakitamba kileleni baada ya kujikusanyia pointi 25, kila timu ikicheza michezo 10.

Nafasi ya tatu katika msimamo wa ligi hiyo inashikiliwa na Singida Black Stars yenye pointi 23 wakati Azam FC yenye alama 21 inafuatia.

Mabingwa hao watetezi walipoteza mechi ya kwanza Jumamosi iliyopita pale walipofungwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC kwenye uwanja huo huo.

Mara ya mwisho Yanga kupata kipigo kikubwa zaidi katika Ligi Kuu ilikuwa msimu wa 2019/20, ilipobamizwa mabao 3-0 dhidi ya Kagera Sugar, mechi ikichezwa Januari 15 mwaka, 2020 kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, wakati huo ikiwa chini la Kocha Mkuu Mbelgiji, Luc Eymael.

Kikosi cha Tabora United kiko chini ya kocha mpya Mkongomani, Anicet Kiazayidi, ambaye amechukua mikoba iliyoachwa na Francis Kimanzi.

Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kurejea tena kuanzia Novemba 21, mwaka huu baada ya kumalizika kwa Kalenda ya Kimataifa ambapo Tanzania itasafiri kuifuata Ethiopia Novemba 16 na baadaye kurejea nyumbani kuwasubiri Guinea.

## Simba: Gari limewaka

INATOKA UK. 24

na tunataka kuendelea kuwa juu," alisema Ahmed.


Ligi hiyo itarejea tena kuanzia Novemba 21, mwaka huu kwa michezo mbalimbali huku mechi za vigogo zilizopangwa kufanyika siku hiyo zimeahirishwa wakati Novemba 23, mwaka huu Azam FC itawaalika Kagera Sugar kutoka Bukoba mkoani Kagera.

Kagera Sugar yenye pointi nane sawa na Pamba Jiji na KenGold yenye pointi tano zinaburuza mkia katika msimamo wa ligi hiyo yenye timu 16.

Michezo
Jumamosi Novemba 9, 2024
Nipashe

## Mbappe atemwa Ufaransa

UKURASA 21



# Gamondi abeba lawama Yanga

●●●Ni kufuatia kipigo cha pili mfululizo, akalia kuti kavu...

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

WAKATI kukiwa na tetesi za kuwekwa kikaangoni na mabosi wake, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema yeye ndio anastahili lawama zote kufuatia kufungwa mabao 3-1 na Tabora United katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi jioni.

Taarifa zilizopatikana jijini jana zinasema viongozi wa timu hiyo walifanya kikao cha dharura na Gamondi kwa lengo la kujadili mwenendo wa timu hiyo baada ya kupoteza mechi ya pili mfululizo.

Chanzo hicho kinaendelea kusema mbali na matokeo mabaya ambayo Yanga imepata na kupoteza pointi sita, inadaiwa Gamondi amekuwa na tabia ya kufanya kile anachoamini yeye na si kusikiliza mahitaji ya viongozi wa klabu hiyo.

"Huenda maamuzi magumu yatafanyika, tuendelee kusubiri," kilisema kwa kifupi chanzo chetu.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mchezo huo, Gamondi, alisema hawakuwa na siku nzuri kutokana na kipigo hicho cha kushtukiza.

"Lawama zote zije kwangu, hatukuwa na siku nzuri, tulitengeneza nafasi hatukuzitumia, kama uliona tulipata penalti lakini hatukuitumia vizuri, sitaki wachezaji wangu walaumiwe, kama kuna lawama zozote basi mimi ndio ninastahili kupewa," alisema Gamondi.

Kocha huyo raia wa Argentina alisema mchezo huo ulikuwa ni kengele kwa Yanga ya kukumbuka ugumu na upinzani uliopo katika

INAENDELEA UK. 23




Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Pacome Zouzoua (kulia), akiwania mpira dhidi ya nyota wa Tabora United, Yacuoba Songne, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi jioni. Yanga ilichapwa mabao 3-1. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA: GARI LIMEWAKA

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kukaa kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba imesema kwa sasa gari limewaka na watahakikisha hawashuki kwenye nafasi hiyo.

Simba inaongoza katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 25, ikifuatiwa na mabingwa watetezi, Yanga wenye pointi 24 na Singida Black Stars ikishika nafasi ya tatu baada ya kujikusanyia pointi 23, kila timu imecheza mechi 10.

Kauli hiyo imetolewa kufuatia Yanga kufungwa mabao 3-1 na Tabora United katika mechi nyingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa juzi, ikikubali kipigo cha pili mfululizo.

Akizungumza jijini, Dar es Salaam jana, Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema wachezaji wa timu hiyo wamedhamiria kupambana katika michezo inayofuata ili kuendelea kujiimarisha katika nafasi hiyo ya kwanza.

Ahmed alisema malengo ya timu yao ni kuhakikisha msimu huu wanatwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambao wanakiu nao.

"Lengo letu ni kuendelea kubaki kileleni, hatujafika hapo kwa bahati mbaya, ni malengo yetu na kujituma kwa wachezaji wetu, tuna kikosi kizuri ambacho kila siku kinazidi kuimarika, tunautaka ubingwa msimu huu," alisema Ahmed.

Aliongeza Simba inapanga kutumia mapumziko ya Kalenda ya Kimataifa ili kujiimarisha na baadaye kuendelea na kasi yao ya kutoa dozi kwa kila timu watakayokutana nayo.

"Tunaenda mapumziko mafupi tukiwa na lengo la kurejea kwa kasi kubwa katika michezo yetu ya Ligi Kuu, hapa gari ndio limewaka, kila mchezo kwetu ni mkubwa

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >